# Nipashe

Alhamisi Desemba 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581538

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Wiki** tatu Malasusa kusimikwa, mtihani wake wa cheo kipya

UKURASA 2

**DCEA** yanasa tani za 'unga' zinazoweka rekodi mpya

UKURASA 3

**Wazazi** wakiri kuwashawishi watoto kufeli darasa la saba

UKURASA 16


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Kituo Sayansi kimekuja na teknolojia kuzalisha mboga bila kutumia udongo

Zimemtia kichefuchefu RPC, ajitosa shule, nyumba za ibada hadi migodini

AHADI YA RAIS & MRADI MAJI ULIKOTOKA ...

Mwaka 2024 waja na zawadi Bwawa la Nyerere kuihakikishia nchi umeme

UKURASA 11



# Kesi ya Gekul yaibua gumzo

• **YATEKA** hisia kortini, DPP akosolewa kuifuta; walalamikaji waandaa rufani... *Ukurasa 2*

# Tishio mgomo: NHIF, hospitali binafsi kukaa meza moja

UKURASA 3




RIPOTI MAALUM

# Mageuzi siku 37, madarasa nyasi hadi majengo kisasa

UKURASA 4

MICHEZO **YANGA YAMNASA MCAMEROON** UK.24 **MAONI** UK.6



Wafadhili wa Taasisi ya Silver Crescent kutoka nchini Uturuki waliotoa huduma ya matibabu ya macho bure kwa wananchi 300 wilayani Muheza, kuchimba visima vitano vya maji na kutoa msaada wa vyakula na fedha kwa wananchi 240 wakifurahia kula tunda aina ya fenesi juzi, wilayani humo mkoani Tanga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kesi ya Gekul yaibua gumzo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JANA ikiwa ndio siku Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, kupandishwa kizimbani, nje ya mahakama kukiwapo umati uliovutwa kushuhudia, ghafla kesi hiyo ikafutwa.

Umati uliokusanyika unaozidi watu 150 na wengine wakizidi kumiminika majira ya asubuhi, wanasheria wa pande zote, mlalamikaji Hashim Ally, anayedai kufanyiwa udhalilishaji, walikuwa mahakamani, isipokuwa Gekul.

Katika mchakato uliochukua wastani wa dakika 15, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario, alipokea kwanza maelezo ya wanasheria na kisha akatamka rasmi kesi hiyo imeondolewa mahakamani, uamuzi uliochukua dakika moja na sekunde 55.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wake Hakimu Kimario, hatua hiyo inatokana na uamuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), akitumia kifungu husika cha sheria kwamba hana nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Ni mazingira ya aina yake nje na ndani ya mahakama, ambako walikuwapo wanaotajwa kuwa mabinti wawili wa mlalamikiwa Gekul. Pia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Abdulaman Kololi na Katibu wa Mbunge huyo.

Awali kabla ya kuingia kizimbani, Gekul ambaye hakuwapo ndani ya chumba cha mahakama, akidaiwa alikuwa katika gari lililofika mahakamani huko na Katibu wake alionekana kuwa na mawasiliano kila mara.

Baada ya kutapakaa taarifa hizo kitaifa, wanasheria ambao nao wamekuwa wakifuatilia kesi hiyo kwa karibu, waliupokea uamuzi huo kwa hisia tofauti, ikiwamo kukosoa alichoamua DPP.

"Kitendo cha DPP kukataa kuendelea na kesi hiyo, kisheria yuko sawa, lakini kwa busara hayuko sawa, kwa kuwa kesi hiyo inafahamika, ilipaswa isikilizwe na mahakama ndio itumike kumsafisha mtuhumiwa," alitamka Wakili wa Kujitegemea, Bashiru Yakubu.

Ni aina ya sauti hizo, ambazo Nipashe ilikutana nazo nje ya chumba cha mahakama kupata maoni ya mapokeo ya uamuzi wa kesi hiyo.

**ILIVYOKUWA KORTINI**

Hakimu Kimario alisema DPP ameiondoa mahakamani kesi hiyo ya udhalilishaji wa kumwingizia chupa sehemu za siri kijana Hashim Ally iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Gekul.

DPP ameiondoa kesi hiyo mahakamani kwa mujibu wa Kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka jana. Hakimu alisema sheria hiyo inampa DPP mamlaka ya kuiondoa mahakamani kesi yoyote ya jinai.

Kesi hiyo Na. 179 ya mwaka huu ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Babati, ilifutwa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi Kimario.

Katika kesi hiyo, mlalamikaji Hashim Ally, alitetewa na mawakili watatu, wakiongozwa na Peter Madeleka. Wengine ni Wakili Thadei Lister na Joseph Masanja. Gekul alikuwa anatetewa na Wakili Efrahim Kisanga.

**NJE YA MAHAKAMA**

Baada ya kutolewa uamuzi huo, Wakili wa Mlalamikaji, Peter Madeleka, alidai kilichotokea ni matumizi mabaya ya sheria, matumizi mabaya ya mahakama na kuidhalilisha mahakama.

Alidai kuwa katika kesi hiyo ya kumdhalilisha Ally, mshtakiwa alitakiwa kufika mahakamani kujibu wito wa mahakama wa Desemba 15, mwaka huu.

"Leo (jana) hii tunapeleka rufani Mahakama Kuu Kanda ya Manyara au ikiwezekana tutakwenda Mahakama ya Rufani ili tupate mwenendo sahihi wa kesi," alidai Wakili Madeleka.

**DPP AKOSOLEWA**

Wakili wa Kujitegemea kutoka Kampuni ya Accuracy ya Kinondoni, Dar es Salaam, Bashiru Yakubu, alisema kwa kuwa kesi hiyo ni jinai, kwa mujibu wa sheria za nchi, mtu binafsi haruhusiwi kuiendesha isipokuwa kwa kibali cha DPP.

"Ndio maana kesi zote huwa zinaandikwa jina la mtuhumiwa dhidi ya Jamhuri kwa sababu mtu akifanya jinai, DPP ndiye anapeleka kesi mahakamani, inasimamiwa na Jamhuri na mlalamikaji anakuwa shahidi kwenye kesi.

Alidai kuna hatari kifungu tajwa cha sheria kilichotumiwa na DPP kuifuta kesi dhidi ya Gekul, kisiwanufaishe watu maskini.

Wakili wa Kujitegemea, Aidan Mbuguye, alidai DPP hana mamlaka ya kuifuta kesi hiyo au kusema kuwa hana nia ya kuendelea nayo kwa kuwa imefunguliwa na mtu binafsi na si ofisi yake.

"Yeye alitakiwa tu akae asubiri aone kama kuna haki itatendeka kwa pande zote mbili na si kusema kuwa hana nia ya kuendelea nayo au kuifuta," alisema.

Mbunge Gekul, akiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, alituhumiwa kutoa maelekezo kwa kundi la vijana kumdhalilisha kwa kumpiga, kumwingizia chupa sehemu za haja kubwa na kumtishia kumpiga risasi mfanyakazi wake, Hashim Ally.

## Tarehe Malasusa kusimikwa ukuu wa KKKT yatangazwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU Mteule wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, anatarajiwa kukabidhiwa rasmi mikoba ya kuliongoza kanisa hilo kwa kipindi cha miaka minne Januari 21, mwakani.

Askofu Malasusa anaingizwa kazini wakati ambao atalazimika kutekeleza maazimio ya mkutano mkuu wa 21 wa KKKT uliopitisha rasmi kuanzishwa mchakato wa kuwa na katiba moja ya kanisa hilo.

Mchakato mzima wa uanzishaji wa katiba hiyo ya KKKT umepewa muda wa mwaka mmoja kufikia lengo hilo.

Ibada maalum ya kuwekwa wakfu Dk. Malasusa ili kuingizwa kazini, itafanyika katika Kanisa la Azania Front lililoko Dayosisi ya Mashariki na Pwani, jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Frederick Shoo, alitangaza nia yake ya kukabidhi kijiti hicho jana katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati akizungumza na diaspora 444 wanaoishi nje ya majimbo matano ya Dayosisi ya Kaskazini.

"Hili la mchakato wa katiba moja ya KKKT, ni jambo kubwa la kihistoria. Ninawahisi waumini wa KKKT popote pale mlipo mwombee jambo hili.

"Mkutano huo mkuu uliwakilishwa na dayosisi zote katika mkutano wa mabadiliko ya katiba ulioitishwa mwezi wa nane (Agosti) mwaka huu, uliazimia kukamilisha jambo hili.

"Uchaguzi huu umeitishwa baada ya mimi kumaliza vipindi vyangu viwili vya miaka minane kikatiba.

"Mnaelewa mzigo huu haukuwa mwepesi, lakini kwa maombi yenu ya kunitia moyo, ninaamini nimeiwakilisha dayosisi yetu vizuri na jina la bwana litukuzwe.

"Pili, niwaombe mwombee sana Mkuu mpya ambaye nitamkabidhi hiki kijiti Januari 21 ili bwana amwezeshe kufanya kazi hiyo, huduma ya bwana ikaendelee kutendeka kama bwana mwenyewe anavyotaka," alisema. Malasusa, ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, alichaguliwa usiku wa manane na wajumbe wa mkutano huo wa KKKT, ulioanza Agosti 20 hadi 25 mwaka huu katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kilichoko Usa River, mkoani Arusha, baada ya mchuano mkali uliompa ushindi katika duru ya tatu.

Askofu Malasusa anarejea tena kwenye nafasi hiyo aliyohudumu kuanzia 2007 hadi 2015, alipomaliza kipindi chake na kumpisha Askofu Dk. Shoo.

Mkuu huyo mpya wa KKKT anakabiliwa na kibarua kigumu cha kuzitafsiri changamoto zilizoko ndani ya kanisa hilo na kuzitatua.

Moja ya mambo yanayomkabili Askofu Malasusa; ni utekelezaji wa mchakato wa katiba mpya ulioridhiwa na kanisa.

Katiba mpya inayosukwa hivi sasa inampa nguvu ya kusimamia dayosisi zote 27, kulinganisha kanisa kutoka dayosisi zote, ambayo kila moja ina katiba yake na kuwa na katiba moja.

Pamoja na mambo mengine, analazimika kutafuta namna ya kumaliza tofauti za kimtazamo miongoni mwa maaskofu wa kanisa hilo.

Pia ana kazi ya kufanya ili mali zote za kanisa, ziwe za umoja wa kanisa, pia kuimarisha zaidi uhusiano wao na serikali.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | RAMADHAN HAMIS NTUZWE | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – VIJIBWENI ,KIGAMBONI | LEHAREL GROUP OF COMPANY | 11/01/2024 |
| 2 | ABBAS RASHID MVITA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI-VINGUNGUTI ,ILALA | LEHAREL GROUP OF COMPANY | 11/01/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# NHIF yaita wamiliki hospitali binafsi, serikali

**Na Joseph Mwendapole**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umewaita wenye hospitali binafsi na serikali kujadili mambo mbalimbali ikiwamo bei mpya zinazotarajiwa kuanza Januari mosi, mwakani.

Juzi Chama cha Wamiliki wa Hospitali Binafsi (APHFTA), kilitishia kuacha kuwahudumia wanachama wa mfuko huo wakidai kuwa hawajashirikishwa kwenye maandalizi ya bei mpya za matibabu.

Katika barua ya mwaliko kutoka NHIF kwenda kwa hospitali za rufani za kanda za serikali, binafsi na za taasisi za dini, Meneja wa NHIF Mkoa wa Kinondoni, Dk. Christopher Lazeck, alisema mwaliko huo ni sehemu ya ushirikishwaji wa wadau mbalimbali kwenye huduma za mfuko.

Kwa mujibu wa barua hiyo, mkutano huo utafanyika Desemba 29, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Barua hiyo ilisema mwaka 2018 NHIF ilianza mchakato wa kuboresha kitita chake baada ya serikali kutoa mwongozo wa matibabu kwa lengo la kuwianisha huduma za kitita cha mafao, mwongozo huo na bei ya soko.

Ilisema kupitia barua yenye kumbukumbu namba EA.35/269/01-A/32 kuhusu dhamira ya mfuko ya kuanza kutumika kwa kitita cha mafao kwa lengo la kupata maoni, NHIF ilikutana na wadau na kupata maoni mbalimbali kwa ajili ya maboresho zaidi.

"Lengo la maboresho ya yaliyofanyika ni pamoja na kuhuisha kitita cha mafao na miongozo ya tiba nchini, kuweka usawa wa ada ya kumwona daktari bingwa kulingana na taaluma na ikama, kuboresha bei za huduma kulingana na hali halisi ya soko," ilisema.

Aidha, maboresho yalilenga kuongeza motisha kwa watoa huduma vikiwamo vituo vya ngazi ya mkoa, wilaya na vituo vya afya na zahanati na kuwezesha huduma za kibingwa kupatikana karibu na wananchi.

Mmoja wa wanachama wa APFTA akizungumza na gazeti hili jana kwa sharti la kutotajwa jina, alisema mkutano huo ni wa kuhalalisha uamuzi uliofanywa kwasababu hakuna kitakachobadilika ndani ya muda huo.

Alisema mkutano unafanyika Desemba 29 ikiwa zimebaki siku mbili tu kuanza kwa utekelezwaji wa bei mpya hivyo kuwaita ni kama kufunika kombe mwanaharamu apite.

Alisema NHIF imeamua kufanya hivyo ikifahamu kuwa watu wengi wako likizo ndani ya nje ya nchi kwa hiyo hawatahudhuria mkutano huo wa Ijumaa.

"Sasa fikiria wanaita watu zikiwa zimebaki siku mbili kuanza kwa bei hizo mpya unadhani kuna kitu kitabadilika ndani ya muda huo kama sio danganya toto, sisi tunaona wanataka wapate cha kusema kwamba tuliwashirikisha," alisema.

Mwanachama mwingine ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema wameshangaa kuona wanaitwa siku mbili kabla ya kuanza kwa bei hizo mpya na kuhoji kwanini waitishe mkutano huo zikiwa zimebaki siku mbili za utekelezaji.

"Hapa naona kama wanatuchezea shere tu kwasababu wameshapanga na watatekeleza kwasasa bei mpya zinaanza Januari mosi wao wanatuita tarehe 29 Desemba siku mbili watabadilisha nini," alihoji bila kutaka kutajwa jina lake.

Juzi wamiliki hao walitishia kugomea kutibu wagonjwa wanachama wa (NHIF), iwapo bei mpya zilizotangazwa na mfuko huo zitaanza kutumika Januari Mosi kama ilivyopangwa.

Kupitia taarifa yao kwa vyombo vya habari, wamiliki hao walisema bei hizo mpya zilipitishwa bila kuwashirikisha na kitasababisha hospitali nyingi kufungwa kutokana na kupata hasara iwapo kitaanza kutumika.

# DCEA yanasa tani za 'unga' zinazoweka rekodi mpya

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imesema katika kipindi cha siku 18 mwaka huu, imekamata dawa za kulevya kilo 3,182 aina ya heroin na methamphetamine katika mikoa ya Dar es Salaam na Iringa.

Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni ya kukamata dawa hizo iliyofanyika kuanzia Desemba 5 hadi 23, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Lyimo, watu saba wamekamatwa wakituhumiwa kuhusika na kiasi hicho cha dawa, wawili kati yao wana asili ya Asia.

Akitoa uchambuzi wa dawa hizo, Lyimo alisema kilo 2,180.29 ni dawa aina ya metgamphetamine na kilo 1001.71 ni aina ya heroin ambazo zilikamatwa wilayani Kigamboni, Ubungo, Kinondoni jijini Dar es Salaam pamoja na Wilaya ya Iringa mkoani Iringa.

"Ukamataji huu umehusisha kiasi kikubwa cha dawa za kulevya ambacho hakijawahi kukamatwa katika historia ya Tanzania tangu kuanza kwa shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya. Hivyo watuhumiwa waliokamatwa ni miongoni mwa mitandao mikubwa ya wauzaji wa dawa za kulevya inayofuatiliwa nchini na duniani," alisema Lyimo.

Alisema kiasi cha dawa kilichokamatwa kilikuwa kimefungashwa kwenye vifungashio vya bidhaa zenye chapa mbalimbali za kahawa na majani ya chai.

Lyimo alisema mbinu hiyo inatumika kurahisisha usafirishaji na kukwepa kubainika.

Alisema dawa hizo endapo zisingekamatwa na kuingia mtaani zingeathiri zaidi ya watu milioni 76 (idadi inayojumuisha na wananchi wa nchi jirani).

"Hivyo ukamataji huu umeokoa nguvu kazi ambayo ingeangamia kutokana na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi."

Alisema DCEA inatoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na mamlaka, mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano unaotokana na wananchi wanaotoa taarifa ya watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Kadhalika, alisema DCEA inatoa onyo kwa watu wanaoendeleza kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya nchini kuacha, badala yake wajikite kwenye biashara halali na imejizatiti kukomesha biashara hiyo kwa kufanya operesheni katika maeneo mbalimbali.


airtel money

TUMA NA KUTOA PESA BILA TOZO

ADA ZA MIAMALA YA AIRTEL MONEY

TOA PESA KWA WAKALA/ATM

| Kutoka TSH | Kwenda TSH | Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato | Okoa Tozo | Unalipa Bila Tozo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 100 | 999 | 200 | 10 | 210 | 10 | 200 |
| 1,000 | 1,999 | 320 | 10 | 330 | 10 | 320 |
| 2,000 | 2,999 | 400 | 10 | 410 | 10 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 604 | 14 | 618 | 14 | 604 |
| 4,000 | 4,999 | 667 | 27 | 694 | 27 | 667 |
| 5,000 | 6,999 | 1,004 | 54 | 1,058 | 54 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 1,056 | 56 | 1,112 | 56 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 1,552 | 102 | 1,654 | 102 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 1,645 | 195 | 1,840 | 195 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 2,156 | 306 | 2,462 | 306 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 2,201 | 351 | 2,552 | | |
| 40,000 | 49,999 | 2,300 | 419 | 2,719 | | |
| 50,000 | 99,999 | 2,600 | 573 | 3,173 | | |
| 100,000 | 199,999 | 3,500 | 707 | 4,207 | | |
| 200,000 | 299,999 | 5,100 | 821 | 5,921 | | |
| 300,000 | 399,999 | 6,200 | 838 | 7,038 | | |
| 400,000 | 499,999 | 6,700 | 982 | 7,682 | | |
| 500,000 | 599,999 | 7,200 | 1,245 | 8,445 | | |
| 600,000 | 699,999 | 7,600 | 1,532 | 9,132 | | |
| 700,000 | 799,999 | 7,600 | 1,700 | 9,300 | | |
| 800,000 | 899,999 | 7,600 | 1,750 | 9,350 | | |
| 900,000 | 1,000,000 | 7,600 | 1,776 | 9,376 | | |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 7,600 | 1,875 | 9,475 | | |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | | |
| 5,000,001 | 10,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | | |

BILA TOZO

TUMA PESA AIRTEL - AIRTEL

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 25 | - | 25 |
| 25 | - | 25 |
| 40 | - | 40 |
| 50 | - | 50 |
| 120 | - | 120 |
| 140 | - | 140 |
| 325 | - | 325 |
| 350 | - | 350 |
| 360 | - | 360 |
| 375 | - | 375 |
| 380 | - | 380 |
| 675 | - | 675 |
| 940 | - | 940 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 2,100 | - | 2,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,250 | - | 3,250 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,000 | - | 4,000 |
| 4,000 | - | 4,000 |
| 4,000 | - | 4,000 |

BILA TOZO

TUMA PESA MITANDAO MINGINE

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 45 | - | 45 |
| 45 | - | 45 |
| 90 | - | 90 |
| 90 | - | 90 |
| 180 | - | 180 |
| 180 | - | 180 |
| 180 | - | 180 |
| 495 | - | 495 |
| 540 | - | 540 |
| 612 | - | 612 |
| 675 | - | 675 |
| 1,125 | - | 1,125 |
| 1,440 | - | 1,440 |
| 1,710 | - | 1,710 |
| 2,070 | - | 2,070 |
| 2,250 | - | 2,250 |
| 2,880 | - | 2,880 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |

BILA TOZO

LIPA KWA AIRTEL MONEY

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 20 | - | 20 |
| 50 | - | 50 |
| 70 | - | 70 |
| 100 | - | 100 |
| 200 | - | 200 |
| 300 | - | 300 |
| 500 | - | 500 |
| 500 | - | 500 |
| 850 | - | 850 |
| 920 | - | 920 |
| 1,000 | - | 1,000 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,700 | - | 1,700 |
| 2,000 | - | 2,000 |
| 2,600 | - | 2,600 |
| 3,000 | - | 3,000 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,500 | - | 4,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,700 | - | 5,700 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |

BILA TOZO

TUMA PESA KWENDA BANK

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 140 | - | 140 |
| 220 | - | 220 |
| 400 | - | 400 |
| 450 | - | 450 |
| 600 | - | 600 |
| 710 | - | 710 |
| 1,000 | - | 1,000 |
| 1,250 | - | 1,250 |
| 1,430 | - | 1,430 |
| 1,430 | - | 1,430 |
| 1,930 | - | 1,930 |
| 2,120 | - | 2,120 |
| 2,780 | - | 2,780 |
| 3,740 | - | 3,740 |
| 4,600 | - | 4,600 |
| 4,700 | - | 4,700 |
| 5,200 | - | 5,200 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 7,500 | - | 7,500 |
| 9,000 | | 9,000 |
| 11,000 | - | 11,000 |

BILA TOZO

KUMBUKA

- Unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa ama kutuma hadi Tsh 5,000,000 kwa siku kama usajili wako umekamilika na Airtel Money.
- Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
- Kuangalia salio la kiasi kwenye akaunti ya Airtel Money ni BURE
- Kuangalia miamala miwili ya mwisho, taarifa ya muamala, muhtasari wa siku iliyopita, muhtasari wa siku, miamala ya mwezi uliopita, utatozwa gharama ya Tsh 50 kwa kila muamala
- Kuwasiliana na Huduma kwa Wateja, Piga 100 bure au tembelea duka lolote la Airtel Money Branch.

FANYA MALIPO KWA AIRTEL MONEY

GePG MALIPO YA SERIKALI · LUKU · VING'AMUZI · MAJI · POLISI · SOLAR · BIDHAA MITANDAONI · MIAMALA YA KIBENKI · TRA · VIKOBA · BRELLA · ARDHI · NDEGE · BIMA · LIPA MITANDAO YOTE

Fanya yote na My Airtel App!
Pakua katika simu yako.

Download on the App Store · ANDROID APP ON Google play

Fanya malipo ya Serikali na bili mbalimbali kupitia My Airtel App

SUMATRA For Competitive, Efficient, Quality and Safe Transport Services · Wizara ya Nishati na Madini · BRELA · Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi · dawasco

Novemba, 2023

HARAKA.SALAMA.BILA MIPAKA.

## NDANI YA SIKU 37

# Mageuzi kutoka madarasa ya nyasi hadi majengo ya kisasa

## -Ni zao la simulizi 'nje-ndani' ya gazeti hili

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

ILIKUWA tarehe 21 ya mwezi uliopita (siku 37 zilizopita), gazeti hili liliporipoti kuhusu madarasa yaliyojengwa kwa nguzo za miti na kuezekwa kwa nyasi katika Shule ya Msingi Magomeni, wilayani Tunduru.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Memeto Mkete, anabainisha kuwa hadi kufikia saa 12 jioni siku hiyo, tayari walikuwa wamepokea maagizo toka kwa uongozi wa halmashauri kujenga madarasa matatu na ofisi moja ya walimu shuleni huko.

Mkete anasema kuwa kabla ya maagizo hayo ya ujenzi wa madarasa na ofisi ya walimu, waliagizwa kubomoa madarasa yenye miundombinu ya nyasi shuleni kwao.

"Kutokana na uhaba wa madarasa, shule yetu ilikuwa na tatizo la kuwa na vyumba vya madarasa vilivyoezekwa kwa nyasi. Juzi kati tuliambiwa tuvichome moto.

"Hili suala (la kuchoma madarasa ya nyasi) lilitokea huko juu kwa maelezo niliyoyapata. Mwalimu Mkuu (Ezekiel Menge) aliambiwa na mamlaka zake za juu kwamba Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru (Chiza Marando) katoa maagizo 'madarasa hayo chomeni moto'.

"Sasa, kwa mujibu wa taratibu za kisheria, mwalimu mkuu ni mdogo kiutendaji, alipopata taarifa hiyo, akanipigia simu akanieleza hayo. Nikamwambia 'sawa kwa sababu maagizo yametoka juu na wewe ni mdogo'. Basi tukapuliza moto yale madarasa," Mkete anasema.

Mwenyekiti huyo anaeleza kuwa kuripotiwa gazetini dosari hiyo ya miundombinu shuleni kwake, kumechangia uongozi wa wilaya kuchukua hatua haraka kuirekebisha.

"Tumekuwa na madarasa ya nyasi kwa muda mrefu, lakini viongozi wa serikali walikuwa wanakuja hapa shuleni kuangalia haya mazingira na hata hayo madarasa ya nyasi walikuwa wanayaona na hawakufanyia kazi.

"Kwa bahati nzuri mwandishi amepiga picha na kuzungumza na sisi viongozi. Tuliyokuwa na uwezo nayo tulimtajia moja hadi lingine.

"Baada ya muda kidogo, ikaja taarifa tunapewa mradi wa madarasa matatu. Nilipohoji kwa Mratibu Elimu Kata, akasema fedha za mradi huo zinatoka serikalini.

"Serikali inanunua vifaa vyote vya ujenzi na kuwalipa mafundi. Nguvu za wananchi ni kuchimba msingi na kupeleka maji kwenye mradi, basi! Kuna siku wanaleta mchanga na matofali hadi usiku," alisema Mkete.

Kujengwa kwa madarasa hayo kunaifanya Shule ya Msingi Magomeni iliyoanza kutoa huduma mwaka 2002, kuwa na madarasa saba.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Marando, katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi Novemba 19, mwaka huu, alikiri kutoa maagizo kubomolewa miundombinu yote ya nyasi katika shule zote za wilayani Tunduru, akisisitiza haikubaliki kisera na ni picha mbaya kwa halmashauri.

Marando pia alisema wanahitaji Sh. bilioni 18 kukabili uhaba wa miundombinu na samani katika shule za msingi 153 za halmashauri hiyo.

**RIPOTI YA CAG**

Magomeni si shule pekee inayokabiliwa na uhaba wa miundombinu na samani. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, anabainisha kuwapo upungufu mkubwa wa miundombinu na samani katika shule nyingi nchini.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6, mwaka huu, CAG Kichere anaeleza kuwa tathmini yake kuhusu miundombinu ya shule za msingi za halmashauri 45 alizozikagua, ilibaini zilikuwa na upungufu wa madarasa 27,316, madawati 158,066, vyoo 56,530 kwa ajili ya wanafunzi na nyumba za walimu 35,684.



Ujenzi wa madarasa na ofisi ya walimu ukiendelea katika Shule ya Msingi Magomeni, wilayani Tunduru. PICHA: MPIGAPICHA WETU

| Miundombinu | Mahitaji | Yaliyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Madawati | 596,872 | 438,806 | 158,066 |
| Vyoo (w'funzi) | 100,630 | 44,100 | 56,530 |
| Nyumba | 45,557 | 9,873 | 35,684 |
| Viti na meza | 63,764 | 33,935 | 29,829 |
| Madarasa | 57,866 | 30,550 | 27,316 |
| Ofisi walimu | 4,997 | 2,731 | 2,266 |
| Vyoo (walimu) | 1,520 | 898 | 622 |
| **JUMLA** | **871,206** | **560,893** | **310,313** |

**Hali ya uhaba wa miundombinu na samani katika shule za msingi za halmashauri 45 nchini. CHANZO: Ripoti ya CAG, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa 2021/22 (Uk. 116).**

Kukiwa na upungufu huo, uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2021/22 uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, unaonesha Sh. bilioni 411.31 zilipotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimali watu nchini kwa mwaka huo wa fedha.

Kwa ujumla, katika uchambuzi wake huo, Taasisi ya WAJIBU inayoongozwa na CAG mstaafu Ludovick Utouh, imebainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, ikisababisha upotevu wa Sh. bilioni 1,770.84/- mwaka 2019/20, Sh. bilioni 4,590.73 mwaka 2020/21 na Sh. bilioni 3,084.55 mwaka 2021/22.

Hii ina maana kwamba, jumla ya Sh. trilioni 9.446 zilipotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika miaka mitatu ya fedha (2019/20-2021/22).

Kiasi hicho kama kingelielekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kingelitosha kujenga vyumba vya madarasa mpya 472,306. Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote.

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77/- | Bil 770.91/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/- | Bil 297.86/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36/- | Bil. 2,015.78/- |
| **Jumla** | **Bil 1,770.84/-** | **Bil 4,590.73/-** | **Bil 3,084,55/-** |

**Mwenendo wa viasharia vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu kwa kipindi cha miaka mitatu. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji; Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu 2021/22 ya Taasisi ya WAJIBU.**

Kimsingi, uhaba wa miundombuni na samani shuleni Magomeni na kwingineko nchini, unakwaza utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

Mpango huo umebainisha malengo muhimu katika sekta ya elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026, ambayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote, malipo yao na makazi kuwa karibu na maeneo ya kazi.

## HABARI KITAIFA

# Morogoro, Tanga zapewa kipaumbele mpango mpya wa kilimo cha karafuu

**Na Mary Geofrey**

MIKOA ya Morogoro na Tanga imepewa kipaumbele kulima karafuu katika mpango wa pamoja wa serikali na wadau wa kilimo kutoka sekta binafsi na taasisi zisizo za kiserikali.

Kuongezwa kwa Mkoa wa Tanga katika ulimaji karafuu kitaifa kumetangazwa katika Mkutano wa Wadau wa Kilimo na Mazingira kutokana na karafuu kuonesha kustawi katika mikoa hiyo miwili. Mkoa wa Morogoro mwaka jana ulizalisha tani 2,000 sawa na nusu ya uzalishaji wa Zanzibar wa jumla ya tani 4,000.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Geoffrey Kirenga, jana jijini Dar es Salaam aliwaeleza wajumbe wa Jukwaa la Wadau wa Kilimo na Mazingira kwamba utafiti umeonesha Mkoa wa Tanga nao unaweza kulima kwa mafanikio zao la karafuu.

Kirenga alisema karafuu ni zao la thamani kubwa, sehemu ya mazao muhimu ya viungo na muhimu katika mazao ya mboga, matunda, mizizi na maua ambayo yana masoko yanayotabirika duniani.

Alisema endapo Watanzania watachangamkia fursa zilizoko katika ulimaji karafuu, uchumi wa mkulima mmoja mmoja na wa Taifa utaimarika na kukifanya kilimo kiwe na tija. "Mazao ya viungo hususani karafuu yamekuwa na soko imara na la uhakika. Sasa bei elekezi ya kilo moja ya karafuu ni kati ya Sh. 14,000 hadi 18,000. "Bei hizi zinaonesha ni jinsi gani zao hili likipewa kipaumbele litakavyokuwa na maana kwa mkulima mdogo na pia likawa ni zao letu lenye tija kubwa katika soko la kimataifa," Kirenga alilieleza jukwaa hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, alisema uingizaji kilimo cha karufuu katika mkakati wa kuinua pato la mkulima una maana kubwa kwa wilaya hiyo.

Alisema kilimo cha karafuu kinawaletea wakulima fursa tele kwa sababu wadau wamejizatiti kuunga mkono kilimo cha zao hilo katika wilaya yao.

"Wilaya yetu imekuwa ikiathiriwa na kilimo kisichokuwa na tija. Kuwapo mazao kama haya ya kimkakati utapelekea kuinua maisha ya mwananchi mmoja mmoja. Tumethibitishiwa kuwa ardhi yetu itastawisha karafuu kama tutazingatia maelekezo ya wataalamu," alisema Nguli. Meneja wa SAGCOT Mkoa wa Morogoro, John Banga, alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa iliyopewa kipaumbele cha kuzalisha kilimo cha mazao ya viungo, hasa karafuu.

"Ndani ya miezi miwili wakulima wamegawiwa zaidi ya miche 150,000 ili waendeleze kilimo cha karafuu. Jambo kubwa na zuri, wapo wadau ambao wamekuja kuunga mkono juhudi hizi za kulima karafuu katika milima ya Morogoro," alisema Banga.

# RC asifu CRDB kuwezesha wananchi huduma kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba amesifu jinsi Benki ya CRDB inavyoshiriki kuwawezesha wananchi kutumia huduma za kidijitali za fedha.

Alitoa pongezi hizo juzi alipokabidhi zawadi kwa mshindi wa samani za ndani wa kampeni ya 'Tisha na Tembocard Tukakiwashe Afcon ya Benki ya CRDB'.

Kindamba alisema si tu kwamba Benki ya CRDB ni mdau mkubwa wa serikali katika utekelezaji miradi ya maendeleo, bali pia inawagusa wananchi moja kwa moja kwa namna tofauti, hivyo kuwainua kiuchumi.

"Sasa hivi dunia imekuwa kijiji kwa kuruhusu mtu kutoka popote duniani kuuza kwa mwingine bila hata kuonana. Haya yote yanawezekana kutokana na mifumo imara ya mawasiliano, hasa malipo ambayo Benki ya CRDB inahamasisha.

"Ninawapongeza kwa juhudi hizi kwani serikali inafanya kila iwezalo kuhakikisha ujumuishaji wananchi kwenye huduma za fedha unakuwa mkubwa kwani ni moja ya njia za kuharakisha maendeleo ya kiuchumi," alisema Kindamba.


Mkuu wa Mkoa huyo alisema Benki ya CRDB pia huendesha kampeni tofauti zinazowashirikisha wananchi na kuwapa fursa tofauti za kuboresha maisha yao, akiitolea mfano kampeni hiyo ya 'Tisha na Tembocard Tukakiwashe Afcon', inayohamasisha matumizi ya kadi kufanya malipo ya huduma na bidhaa katika maeneo mbalimbali kwa kutoa zawadi mbalimbali kwa wateja wake.

"Dada Fatima Mwatime Nundu amefungua pazia la washindi wa zawadi za kampeni ya 'Tisha na Tembocard Tukatishe Afcon' kwa mkoa wetu wa Tanga, hivyo ninaamini wateja wengine wa Benki ya CRDB wataendelea kutumia kadi zao kufanya miamala ili tupate mwanamichezo mmoja atakayekwenda kutuwakilisha Ivory Coast," alisema Kindamba.

Fatima ni mshindi wa kwanza wa seti ya sofa yenye thamani ya Sh. milioni nane katika kampeni ya 'Tisha na Tembocard Tukakiwashe Afcon', inayoendeshwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na kampuni ya kimataifa ya Visa inayowawezesha watu kufanya malipo kwa kutumia kadi popote ulimwenguni.

Kwa kushirikiana na serikali, Kindamba alisema: "Benki ya CRDB imetujengea madarasa mawili pamoja na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi ya Walemavu Chuda iliyoko Tanga Mjini.

Akielezea kampeni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kadi wa Benki ya CRDB, Farid Seif alisema ilizinduliwa Novemba 2, mwaka huu na itadumu mpaka Februari 2, mwakani ikitoa zawadi za aina tofauti zinazojumuisha samani za ndani, vifaa vya kielektroniki mfano runinga, friji na 'home theatre' pamoja na tiketi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia fainali ya Kombe ya Mataifa Huru Barani Afrika (Afcon).




Mshindi wa pesa taslimu Sh. milioni 10 kupitia kampeni ya Vodacom Tanzania PLC inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', Juliana Lukwaro (katikati), akishikiria mfano wa hundi aliyokabidhiwa na Masta Shangwe (mwenye kofia ngumu) na kusindikizwa na msanii wa Bongo Flava, Dogo Janja (mwenye rasta) pamoja George Venanty, Meneja wa Vodacom Kanda ya Kaskazini (mwenye miwani) katika viwanja vya Stendi Kuu mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TASAF imeonesha dhati ya kukomboa kaya maskini

**MPANGO** wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), ulianzishwa mwaka 2000 ukiwa ni mikakati ya Serikali ya Tanzania ya kupunguza umaskini katika kaya zinazoishi maisha duni nchini.

Utekelezaji wa mpango huo umegusa mikoa mbalimbali ya nchi kwa kuhusisha viongozi wa serikali za mitaa katika kutambua wananchi wanaoishi katika kaya maskini na kuorodheshwa kwenye mpango huo.

Utambuzi wa kaya za TASAF hufanyika kwa uwazi kupitia mikutano mikuu ya vijiji na mitaa kwa kutumia sifa za kaya maskini sana katika maeneo husika kabla ya kuchakatwa kwenye mifumo ya kompyuta ili kuzipata kaya zinazokidhi vigezo vya umaskini kama vinavyotambuliwa na Benki ya Dunia.

Baadhi ya sifa za kaya maskini ni zile zisizokuwa na uwezo wa kupata milo mitatu kwa siku, zenye watoto wanaoishi katika makazi na mazingira duni/hatarishi na zinazoshindwa kugharamia huduma za msingi hususani za afya na elimu.

Mafanikio ya mpango huo yanaonekana baada ya kaya nyingi zilizoingizwa kwenye orodha ya kupata ruzuku ya kuwezeshwa kujinasua katika umaskini kuanzisha miradi inayowawezesha kupata mahitaji muhimu ya kibinadamu.

Jukumu la TASAF katika kuziwezesha kaya maskini kupitia mpango huo ni kuwa na miradi inayoweza kuwanasua katika umaskini na kuweza kujisamamia wenyewe kwa kufanya miradi endelevu.

Wanufaika wa Mpango huo wameonesha dhahiri jinsi fedha wanazopewa na TASAF zilivyowasaidia kuboresha kaya zao kwa kufanikiwa kuwa na miradi yao wenyewe ya ufugaji, kumiliki mashamba na kujenga nyumba zilizoezekwa kwa bati.

Kabla ya kuingizwa katika mpango huo, walikuwa wakitafuta kipato angalau cha kuweza kupata mlo mmoja kwa siku kwa kufanya vibarua vya kulima katika mashamba ya watu.

Familia hizo zilishindwa kupeleka watoto wao shule kwa kutokuwa na uwezo wa kuwanunulia mahitaji muhimu kama sare na vifaa vinavyohitajika darasani.

Wazee ndio walikuwa waathirika wakubwa kwa kubwagiwa wajukuu na watoto wao ambao hukimbilia mjini kwa kisingizio cha kutafuta kazi, bila kupelekewa msaada.

TASAF imekuwa mkombozi kwasababu sasa wajukuu wanakwenda shule kupitia miradi iliyoanzishwa na bibi/babu zao ya ufugaji wa kuku, mbuzi, nguruwe na ng'ombe ambao wakiuzwa fedha zinasaidia kununulia mahitaji muhimu na zinazobaki zinaendeleza miradi mingine.

Wengi wa wanufaika wa mpango huo wanaofuatiliwa kuangaliwa maendeleo yao, wanakutwa wakiishi maisha yenye furaha kutokana na kuwa na uhakika wa kupata kipato kupitia miradi waliyoianzisha.


Kupitia miradi hiyo wameanzisha vikundi vyao vya kuweka na kukopa ambavyo vinawasaidia kukopa pesa na kuanzisha miradi mingine inayowapa uhakika wa kusimama wenyewe wanapokuwa wamefaulu kutoka kwenye mpango huo ili kuwezesha kaya nyingine maskini kujiunga.

Baadhi ya wanufaika wamekuwa na uwezo wa kuanzisha biashara za maduka madogo yanayouza bidhaa muhimu na kufikiria kuanzisha maduka ya kuuza bidhaa za jumla.

Wanufaika wengine wameamua kujiunga na kununua shamba ambalo linawaingizia kipato kupitia miti wanayovuna na kila mwanachama kuwa na uwezo wa kumiliki nyumba yake mwenyewe ya kuishi.

Wanufaika wenyewe wanamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupitia serikali anayoingoza kwa kuendeleza mpango huo ambao unaendelea kuwakomboa wananchi wengi waliokuwa katika hali ya umaskini wa kutisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera HELSB kuendeleza yake Rais, tumeona vipaumbele vipya vinne kwa wasomao stashahada

Na Christina Mwakangale

**BODI** ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini (HESLB), imeongeza programu za stashahada katika kipaumbele vinne vilivyo na makundi ya kozi tofauti ndani yake, kwa wanafunzi wa kozi hizi kunufaika na mikopo.

Awali, vipaumbele vilivyotangazwa na serikali kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda vilikuwa sita, hivyo kwa idadi hiyo mpya ni kwamba sasa ni maeneo 10 ya mikopo hiyo kwa kozi mbalimbali.

Ninaipa kongole serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza vipaumbele na kufikia 10 huku ndani yake kukiwa na maeneo ya kozi zisizopungua 19.

Nipashe ya Oktoba 12, mwaka huu, ikiwa ni wiki moja tangu Oktoba 4 mwaka huu, serikali ilipotangaza kuanza kutolewa kwa mikopo kwa mara ya kwanza nchini kwa wanafunzi wa diploma katika vipaumbele vya masomo sita.

Kupitia ukurasa huu, Nipashe ilieleza umuhimu wa kuongezwa kwa vipaumbele hasa zinazotegemewa zaidi katika jamii, ikiwamo kilimo.

Ilieleza pia umuhimu wa kupatiwa mikopo, wanafunzi wa stashahada wa kozi mpya zinazokwenda na mazingira ya sasa kama vile ya kiteknolojia husasan katika sekta ya kilimo, mifugo, fedha, maji, elimu, nishati na madini.

Wiki hii, Desemba 25, mwaka huu, tovuti ya HESLB, ilitangaza kwamba zimeongezwa ikiwa ni TOLEO LA PILI' la 'Mwongozo wa Utoaji Mikopo ya Elimu kwa Wanafunzi wa Stashahada kwa mwaka 2023-2024.

Awamu ya kwanza ya utoaji mikopo hiyo ilipotangazwa na Prof. Mkenda, ni kwamba vipaumbele vipya kwenye elimu vya kupatiwa mikopo ni katika maeneo sita, kwa wanafunzi wa stashahada (diploma), zikitengwa Sh. bil 48.

Prof. Mkenda, alisema fungu hilo ni kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi 8,000 wa stashahada, watakaofanyiwa udahili katika mwaka wa masomo 2023/24.

Kwa mujibu wa waziri huyo, uamuzi huo ni marekebisho ya sheria ya HESLB ya mwaka 2017. Hii ni mara ya kwanza kwa HESLB kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada.

Ikumbukwe, huo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutaka wanafunzi wa vyuo vya kati kunufaika na mikopo ya serikali, ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya Afrika kuhusu rasilimali watu.

Awali mikopo hiyo ilikuwa katika vipaumbele sita na mahsusi kwa wanaosoma; Afya na Sayansi Shirikishi; Elimu (Stashahada ya ualimu wa masomo ya fizikia, hisabati na amali; Usafiri na Usafirishaji); Uhandisi wa Nishati; Madini na Sayansi ya Ardhi; Kilimo na Mifugo.

Na wiki hii, serikali imeongeza vipaumbele vinne, vilivyo na makundi ya kozi kadhaa ndani yake. Vipaumbele hivyo ni Stashahada kwenye Madini na Sayansi ya Ardhi; Uhandisi; Kilimo na Mifugo; Usafirishaji na Logistiki.

Aidha, vipaumbele hivyo vipya vinne mchanganuo wake ni wanafunzi wa Stashahada ya Jiolojia na Uchunguzi wa Madini; Stashahada ya Sayansi ya Jiolojia ya Petroli na Utafutaji; Stashahada ya Upimaji Ardhi na Migodi.

Kadhalika, Stashahada ya Usafiri na Logistiki; Stashahada ya Usafiri wa Baharini na Sayansi ya Nautikali (Nautical Science).

Kozi nyingine zinazopewa kipaumbele katika mikopo ni, Stashahada ya Usafirishaji na Usimamizi wa Usafirishaji; Stashahada ya Usimamizi wa Usafirishaji na Ugavi.

Pia ni Stashahada ya Kilimo na Mifugo; Usimamizi wa Ardhi ya Mifugo na Udhibiti wa Ndege aina ya 'Tsetse Fly' kwenye Mifugo; Stashahada ya Teknolojia ya Uzalishaji wa Miwa.

Kwenye uhandisi ni Stashahada ya Teknolojia ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi; Stashahada ya Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira; Stashahada ya Usanifu wa Majini na Uhandisi wa Pwani.

Kadhalika, Stashahada ya Uhandisi wa Uchakataji wa Madini na Stashahada ya Uhandisi wa Madini.

HABARI KITAIFA

# Pinda aasa matumizi bora ardhi, asema haiongezeki

**Na Munir Shemweta, MLELE**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda amewataka Watanzania kuhakikisha wanakuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo kwa kuwa ardhi iliyopo haiongezeki wakati idadi ya watu inazidi kuongezeka.

Alitoa angalizo hilo jana nyumbani kwake Kibaoni, Halmashauri ya Mpimbwe, mkoani Katavi katika hafla maalum ya chakula aliyowaandalia wananchi na viongozi wa jimbo lake kusherehekea Sikukuu ya Krismasi.

Katika hafla hiyo iliyohudhuriwa pia na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, Naibu Waziri huyo alisema kuwa wakati serikali ikiandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Watanzania wanatakiwa kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi huku wakielewa changamoto kubwa iliyo mbele yao ni kuwa ardhi haiongezeki.

"Miaka 25 inayokuja lazima tufikirie hizi hekta na ekari tulizopewa na Mungu ikaitwa Tanzania zinatushaje itakapofika miaka hamsini ijayo? Kwahiyo, ni sisi ndiyo tutakaopanga tutumiaje maeneo yetu.

"Kila mtu akikaa ajue ardhi ni yake na ndugu zake, hivyo tuishi kwa amani na tusigombane, hakuna namna! Tutakachokifanya katika eneo hili ni lazima tukubaliane namna ya kuitumia ardhi ndogo katika ongezeko kubwa la watu," alisema.

Akizungumzia shughuli za maendeleo kwenye jimbo lake la Kavuu, Naibu Waziri aliwaambia wananchi wake kuwa jimbo hilo kwa sasa limepiga hatua kubwa kulinganisha na miaka ya nyuma kwa kuwa serikali imewezesha utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo, hata ile ambayo haikutajwa kwenye ilani ya CCM na kutolea mfano ujenzi wa zahanati, shule na miundombinu mingine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, Shamimu Mwariko, alisema wananchi wa Mpimbwe kama wanataka halmashauri yao ifanane kimaendeleo na halmashauri zilizopiga hatua kubwa kimaendeleo, wahakikishe wanawashika viongozi wanaofanya uamuzi wa kimkakati.

"Kama kweli mna lengo la kusema sasa sisi Mpimbwe iwe inafanana na eneo fulani, shikeni viongozi wanaofanya uamuzi kimkakati, utekelezaji wao, mipango yao ni kuhakikisha wanafungua njia watu waweze kupita njia hizo, ndio kazi ya kiongozi yeyote duniani," alisema Shamim.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa na Waziri Mkuu mstaafu, Pinda, alimtaka Mbunge wa Kavuu ambaye ni mdogo wake kuwa karibu na wananchi wakati wote wa juhudi mbalimbali za kuliletea maendeleo jimbo hilo. "Hoja kubwa ya wananchi unaowaongoza ni uhusiano, mnaishije? Kila aliyesimama amekupa sifa, ni jambo zuri! Kazi yako sasa ni kutoharibu sifa, kaza uzi na jishushe kadri inavyowezekana na watu wote ni wako, hata wale mliopingana," alisema Pinda.

Naibu Waziri Geophrey yuko jimboni kwake katika Halmashauri ya Mbimbwe kwa lengo la kujumuika na wananchi kusherehekea nao sikukuu ya Krismasi.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akizungumza wakati wa hafla maalum ya chakula alichowaandalia wananchi na viongozi wa jimbo lake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati matumizi mbolea kuongezewa wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TANZANIA inatumia kati ya tani 300,000 hadi 600,000 za mbolea aina mbalimbali kwa mwaka huku lengo likiwa tani milioni moja kwa mwaka.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Morogoro, Dk. Rozalia Rwegasira, alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya udhibiti ubora wa mbolea nchini.

Mafunzo hayo yaliratibiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na kushirikisha washiriki 20 kutoka sekretarieti za mkoa na mamkala za serikali za mitaa.

Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Mwanza, Njombe, Simiyu, Singida, Tabora na Rukwa.

"Katika miaka mitano iliyopita Tanzania imekuwa ikitumia kati ya tani 300,000 na 600,000 za mbolea aina mbalimbali kwa mwaka," alisema Dk. Rwegasira.

Alisema mkakati wa kuongeza matumizi ya mbolea kwa sasa una umuhimu wa pekee hasa ikizingatiwa serikali imetenga bajeti ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima kuanzia msimu wa mwaka 2022- 2023 na msimu wa 2023-2024.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Mkoa wa Morogoro, alisema hatua hiyo imewezesha wakulima kupata na kutumia mbolea bora kwa gharama nafuu.

Dk. Rwegasira, alisema juhudi za serikali zinalenga kuongeza tija ya uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula, kuwezesha upatikanaji wa malighafi za viwanda, ukuaji wa sekta ya kilimo na kuimarisha uchumi kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, katika hotuba yake iliyosomwa na Meneja wa Uhusiano, Mawasiliano na Elimu kutoka Mamlaka hiyo, Matilda Kasanga, alisema kwa mujibu wa sheria ya mbolea, mamlaka imepewa jukumu la kusimamia ubora wa mbolea.

Joel alitaja jukumu ni pamoja na kudhibiti ubora wa utengenezaji, uingizwaji, usafirishaji nje ya nchi, uuzaji na utumiaji wa mbolea nchini.

Alisema, mafunzo hayo yamewajengea uwezo wa kusimamia ubora na kufanya ukaguzi kudhibiti ubora wa mbolea na usimamizi wa mfumo wa ruzuku ili kuimarisha upatikanaji wa mbolea bora kwa wakulima itakayowawezesha kuongeza uzalishaji na tija.

Alitaja eneo lingine ni kufahamu sheria, kanuni na taratibu zinazotumika katika tasnia ya mbolea nchini, mfumo wa kidijitali wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku.

Aliwataka wakati wote wa majukumu yao wakiwa wakaguzi wa mbolea kutenda haki ili biashara ya mbolea ifanyike katika mazingira wezeshi kwa pande zote.

Wahitimu wa mafunzo hayo, Upendo Chaula kutoka Jiji la Mwanza pamoja na Evetha Lyatuu kutoka Halmashauri ya Mji wa Babati kwa nyakati tofauti walisema mafunzo yao yamewajengea uwezo mkubwa tofauti na hapo awali.

Chaula alisema pia washiriki kutoa elimu kwa wakulima watumie matumizi sahihi ya mbolea kwa kupata ushauri kutoka kwa maofisa ugani maeneo yao ya uzalishaji ili kupata mavuno yenye tija.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Makamu Rais ahimiza kutunza uoto wa asili

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ili kuendelea kuwapo rasilimali ya maji ardhini Zanzibar, ni lazima kuchukuwa hatua na kutilia maanani uhifadhi wa mazingira, kupanda miti na kutunza uoto wa asili uliopo.

Othman aliagiza hayo jana huko Masingini, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja alipofungua mradi wa Uimarishaji na Uhuishaji wa Mfumo wa Usamabazaji Maji Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Alisema kufanya hivyo ni kuiendeleza rasilimali hiyo iendelee kuwapo na kuwanufaisha Wazanzibari na kwamba utunzaji wa mazingira ndio unaozalisha maji.

Makamu wa Rais alisema ni jukumu la kila mwananchi na viongozi katika ngazi mbalimbali kutunza mradi huo kimazingira na kimiundombinu ili kuhakikisha unakuwa wa watu wote na kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Alisema ulinzi wa miradi ya aina hiyo ni jukumu la watu wote na kila mmoja ana wajibu wa kushirikiana kuulea ili uwe endelevu na kuwa na manufaa zaidi kwa wananchi.

Othman alisema kuwa katika kutilia mkazo utunzaji mazingira, serikali kupitia ofisi yake itazindua mradi mkubwa wa upandaji miti katika visiwa vyote vya Unguja na Pemba, hatua aliyoitaja inapaswa kuungwa mkono na kila mwananchi na viongozi ili kurejesha Zanzibar ya kijani.

Makamu wa Rais pia aliwataka wananchi kuhakikisha wanalipa bili za maji kwa kuwa kufanya hivyo ni kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelipa umuhimu mkubwa suala la maji kwa kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji miradi ya aina mbalimbali ya maji.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph John Kilangi, alitahadharisha wananchi wanaounganishiwa na watakaounganishwa maji kuhusu uchezeaji wa mita.

Alibainisha kuwa wananchi milioni 1.5 wataunganishwa kwenye mfumo wa kisasa wa mita na kuwataka wananchi wote kuendelea kuitunza miundombinu na kuwa na subira kwa kuwa serikali inaendelea na mipango ya kukamilisha malipo ya vipando kwa waliopitiwa na mradi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Dk. Salha Mohammed Kassim, alisema mradi huo umegharimu Dola za Marekani milioni 92.18 na utekelezaji wake ulianza Aprili, 2020.




Wakazi wa Wilaya ya Muheza, Tanga, wakiangalia katapila lililotitia kwenye matope wakati likifanya kazi ya kusafisha mto Amtico eneo la Kwamtiga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Mbunge aunda kamati kupambana ukatili kijinsia

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Ilemela mkoani Mwanza, Dk. Angelina Mabula, ameunda kamati za kupinga ukatili wa kijinsia ndani ya Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) wilayani humo ili kukomesha vitendo hivyo.

Aidha, mbunge huyo ameahidi kushirikiana na wadau mbalimbali katika vita hiyo, wakiwamo viongozi wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamiii Tanzania (SMAUJATA), Kanda ya Ziwa.

Alisema hayo katika mkutano maalum wa CCM Wilaya ya Ilemela, uliofanyika Pasiansi juzi na kufafanua kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia viko nje na ndani ya umoja huo.

"Ni muhimu kupambana na vitendo hivi ndani ya umoja wetu pia, hivyo nimeunda kamati ya kupinga ukatili wa kijinsia na tutashirikiana na wadau wengine kama SMAUJATA," alisema Dk. Angelina.

Katibu wa SMAUJATA, Kanda ya Ziwa, Hashim Ramadhan, aliwataka wanachama wa umoja huo kuwa walezi wazuri wa watoto na kuwaepusha na utandawazi unaosababisha mmomonyoko wa maadili.

Ramadhan alisema, SMAUJATA imekuwa ikitoa elimu ya madhara ya ukatili wa kijinsia kwa makundi mbalimbali wakiwamo wanasiasa, katika maeneo mbalimbali ya kanda hiyo.

"Nasi tunaahidi kumpa ushirikiano mbunge kwa uamuzi wake wa kuunda kamati ya kupinga ukatili wa kijinsia ndani ya umoja huu, kwani kazi yetu itakuwa inafanana," alisema Ramadhan.

Aidha, alisema hatua aliochukua mbunge huyo ya kuunda kamati za ukatili ndani ya UWT, inalenga kuunga juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kupambana na vitendo hivyo.

"Rais wetu pamoja na Waziri Dk. Dorothy Gwajima na Mwenyekiti wa SMAUJATA, Sospeter Bulugu, mwanzilishi wa kampeni hii, ni vinara wanaotupa nguvu ya kujitoa kwa ajili ya jamii yetu," alisema.

Alisema kupitia viongozi hao, yeye na wenzake wanafikisha elimu ya kupambana na ukatili wa kijinsia ili kulinda watoto majumbani na shuleni.

"Wito wangu ni kwamba, tuendelee kuungana kwa kuwafichua wote wanaotenda vitendo vya ukatili na kutumia pesa zao na kuwafunga midomo waathirika na kusababisha wasitoe ushirikiano," alisema.

Alisema, vita hiyo ni ngumu kwa kuwa baadhi ya watenda maovu ni watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha na mashujaa wa kampeni hiyo wataendelea kupambana nao.

# Mawakala wanaouza mbegu za kuchakachua kukiona

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imesema haitamfumbia macho mtu atakayejaribu kucheza na tasnia hiyo kwa kuuza popote mbegu zisizokidhi ubora na atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Mkaguzi Mwandamizi TOSCI, Emmanuel Mwakatobe, alisema hayo jana wakati akiongea na waandishi wa habari kuwa wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka ya mawakala ili mkulima apate mbegu bora.

"TOSCI inatoa wito kwa yeyote anayetaka kufanya biashara ya mbegu, kama unapenda kukaa salama usicheze na mbegu, mtu yeyote anayetaka kufanya biashara Tanzania ahakikishe anafanya biashara sahihi kwa kufuata kanuni," alisema.

Alisema kwa sasa faini imeboreshwa na mtu atakayebainika kuuza mbegu feki atalipa faini Sh. milioni 500 kwa kosa la kuleta udanganyifu kwa wakulima wa kitanzania.

Mwakatobe alisema tayari mawakala kadhaa wameshapewa onyo na wanaendelea na taratibu za kuwafikisha mahakamani.

Aidha, mawakala wa mbegu nchini wanapaswa kusimamia misingi, taratibu na kanuni za uuzwaji mbegu kwa kuzingatia ubora ili kuleta ongezeko la matumizi ya mbegu bora na kufanya kilimo chenye tija nchini.

Aliwaasa wakulima kuacha tabia ya kununua mbegu kwenye magulio na minada kwa sababu kufanya hivyo kunarudisha nyuma maendeleo ya kilimo nchini.

"Mbegu zilizothibitishwa ubora huuzwa kwa mawakala waliopo nchini huku zikiwa na lebo maalum ya kuthibitisha ubora kutoka TOSCI, hivyo mkulima unaponunua mbegu hakikisha unapata iliyo kwenye kifungashio maalum huku ikiwa na lebo zinazotambulika ikiwamo ya TOSCI ili kuwa na uhakika wa kilimo na kujiepusha na kilimo cha mazoea cha kupata sawa na kukosa sawa," alisema Mwakatobe.

Alisema zaidi ya maduka 800 ya mawakala wa mbegu yameshakaguliwa kwenye maduka kwa kuthibitisha ubora wa mbegu nchini.

Naye mmoja wa wakulima wa mahindi kutoka tarafa ya Mikese, wilayani Morogoro, Neema Sawere, alipongeza TOSCI kwa hatua ya kufanya ukaguzi mara kwa mara kwenye maduka ya mbegu na kuwasaidia kupata zilizo bora kwa ajili ya kuendeleza kilimo chenye manufaa kwao.

Sawere alisema mbegu bora zinawasaidia kupata mazao mengi na bora shambani kutokana na ushauri wa kitaalamu ikiwamo matumizi ya pembejeo na kusafisha shamba kwa wakati.



# Dk. Shoo: Huduma za afya hospitali za kanisa haziko sawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema kanisa hilo limegundua 'kusuasua' kwa usimamizi wa utoaji wa huduma za afya katika hospitali zake za Dayosisi ya Kaskazini.

Amesema kutokana na hali hiyo, dayosisi hiyo inalazimika kuongeza nguvu ya maboresho na uwekezaji ili kurejesha huduma stahiki.

Dk. Shoo, ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, aliyasema hayo jana katika Mji wa Moshi, wakati wa mkutano mkuu wana dayosisi hiyo wanaoishi nje ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Hospitali hizo ni Marangu, Machame na Karatu, ambazo zimetoa mchango mkubwa kwa jamii.

"Kama kanisa tumeona tunawajibu wa kuzikabili changamoto hizo kwa kuboresha huduma za afya zinazotolewa na hospitali zetu.

"Na kwa kuanzia, uongozi wa dayosisi umeimarisha bodi za usimamizi kwa kuweka utaalamu zaidi na kuwajengea uwezo wa uongozi."

Kwa mujibu wa Askofu Dk. Shoo, katika Hospitali ya Machame yamefanyika maboresho mbalimbali hasa upande wa ICU (Chumba cha Uangalizi Maalum) na OPD (Jengo la Wagonjwa wa Nje).

"Pia kwa kushirikiana na wahisani wa nje, tumepata ambulance mpya (gari la wagonjwa) kutoka Mission One World, yenye thamani ya Sh.milioni 140," alisema.

Kwa upande wa Hospitali ya Machame, KKKT imesema imepata Sh. milioni 146, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura na tayari limekamilika.

Aidha, kuna mashine mpya ya X Ray yenye thamani ya Sh.milioni 180,000 na ukarabati wa ICU kwa Sh.milioni 33 kutoka kwa marafiki wa Hospitali ya Machame.

Pamoja na mambo mengine, Askofu Dk. Shoo, alisema tayari wameingia ushirikiano na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, ambapo kwa sasa hospitali zote tatu zinapokea madaktari wanaotoa huduma za kibingwa.

Akifafanua kuwa kutokana na ushirikiano huo imeonekana kuna uhitaji mkubwa wa kupata vifaa tiba vya kisasa na dawa na madaktari hao wa KCMC ili waweze kutumia taaluma yao ipasavyo.

"Tumeona iko haja kubwa tuweke nguvu katika kutafuta vifaa tiba vya kisasa na dawa katika Hospitali ya Marangu ili kuendeleza kutoa huduma bora zaidi, makadirio kwa ajili ya kutimiza malengo yetu ni shilingi milioni 500."

# Sababu wananchi kukabiliwa na utapiamlo zatajwa

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (BOMBO), imetaja sababu ya wananchi mkoani humo kukabiliwa na ugonjwa wa utapiamlo kwamba ni kinamama kushindwa kunyonyesha watoto kwa ukamilifu ndani ya miezi sita tangu wanapojifungua.

Akizungumzia tatizo hilo jana, Ofisa Lishe wa Hospitali hiyo, Mariam Mwakasala, alisema hali hiyo ndiyo inayochochea kuongezeka kwa athari za lishe na udumavu dhidi ya watoto mkoani hapa.

Alisema idadi kubwa ya kinamama wanapotoka kujifungua kwa njia ya upasuaji au njia ya kawaida, hupewa ushauri kwamba baada ya saa moja ni muhimu kuwanyonyesha watoto bila kuwapa kitu chochote isipokuwa dawa.

"Kwa kweli tunatoa elimu ambayo inakwenda sambamba na elimu ya ulaji bora kwa mama ili aweze kutoa maziwa ya kutosha kwa mtoto kwa sababu changamoto kubwa tunayopata utakuta mama amejifungua mtoto ana afya nzuri tu lakini njia anayomnyonyesha inaweza kusababisha asikue vizuri kwa sababu hamnyonyeshi vizuri kutokana na kutokula vizuri," alisema.

Aidha, alisema mwisho wa siku hali hiyo inasababisha kutokana na mama kutokuwa na maziwa ya kutosha na hatimaye kuanza kumchanganyia na kumpa vyakula ikiwamo uji, jambo ambalo linaweza kusababisha utapiamlo kwa mtoto. "Mwisho wa siku ukiangalia takwimu za wenye utapiamlo zinaanzia kwa mama anaposhindwa kumnyonyesha mtoto vizuri kwa sababu tunapomwambia mama anyonyeshe kwa kipindi cha miezi sita ya bila kumpa chochote tunategemea ile kwamba mtoto ataweza kunyonya maziwa ya mama na utumbo wake upo tayari kusaga maziwa ya mama tu," alisema. Alisema ndiyo maana hawashauri kuwapa watoto maziwa ya kopo ingawa yanakaribiana na virutubisho vinavyopatikana kwenye maziwa ya mama ikiwamo kutoa ushauri kwa kinamama wahakikishe wanakula vizuri ili waweze kupata maziwa ya kutosha.

Akizungumzia suala hilo, Mkazi wa Jiji la Tanga, Omari Fundi, alisema kuna umuhimu mkubwa wa wajawazito wakawa wanapewa elimu ya umuhimu wa kuwanyonyesha watoto wao pindi wanapozaliwa ili waweze kulia vizuri.

Alisema: "Lakini ni muhimu sana wakawanyonyesha maziwa watoto kwa kipindi cha miezi sita kwani hapo ndipo wakati muhimu wa watoto kukua."



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Remidius Mwema (wa tatu kushoto), akikabidhiwa nyaraka na mtangulizi wake Mbaraka Batenga ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Polisi walalamikiwa kutomkamata mtuhumiwa ubakaji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKAZI wa Negamsi katika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Mwajuma Mwilu, amelituhumu Jeshi la Polisi kwa kushindwa kumkamata na kumfikisha mahakamani kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, mtuhumiwa wa kesi ya kunajisi na kumwambikiza Virusi Vya Ukimwi, mwanafunzi wa darasa la tatu.

Mtuhumiwa huyo, Mussa Shaban (40), anatuhumiwa kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka 13.


Kwa mujibu wa Mwilu, licha ya kuripoti tukio hilo katika Kituo cha Polisi Babati, mwaka mmoja uliopita, mpaka kufikia sasa, mtuhumiwa huyo anaendelea kutamba mtaani katika Jiji la Mwanza, hajakamatwa wala kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

"Mtoto wangu alinajisiwa mwaka jana mwezi wa Novemba ila mpaka leo, kesi haipelekwi mahakamani. Sielewi shida ni nini na mtuhumiwa ametoroka yupo Mwanza," alisema mama huyo.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, alisema tayari ameshaelekeza kutafutwa kwa jalada la kesi hiyo na hatua zaidi kuchukuliwa.

"Lakini kana kwamba haitoshi, nimetoa maelekezo kwa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa, waongeze makachero kutoka wilayani kwa ajili ya kumsaka mtuhumiwa ili afikishwe mahakamani," alisema Kamanda Katabanzi.

Tuhuma kuhusu mwanafunzi huyo kunajisiwa na kisha Jeshi la Polisi kudaiwa kukalia uchunguzi na jalada la kesi hiyo, zilipelekwa kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.



# Wafanyabiashara Soko la Namanga walia ubovu wa miundombinu

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Namanga katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamemwangukia mbunge wao, Jumanne Kishimba ili aboreshe miundombinu ya soko hilo.

Wafanyabiashara hao walidai kuwa licha ya kulipa ushuru kwa wakati, lakini mazingira yamekuwa hayaendani na fedha wanazolipa hali inayowapotezea wateja.

Walitoa kilio hicho juzi walipotembelewa na mbunge huyo, lengo kuu likiwa ni kusikiliza na kutatua kero zao ili kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira rafiki na kulipa ushuru unaoendana na mazingira.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bwire Stanslaus, alisema soko hilo kwa muda mrefu mazingira yake yameharibika hususani meza za biashara na kuomba mbunge kuingilia kati na kuboresha mazingira hayo.

Aliomba fedha zinazokusanywa sokoni hapo zitumike kuboresha ili kuondoa malalamiko baina yao na serikali kwani eneo hilo ndilo linaloendesha maisha yao. Mfanyabiashara mwingine, Baraka Boniphace alisema, barabara inayoingia sokoni hapo ni mbovu hali inayowafanya kushindwa kufikisha bidhaa zao sokoni kwa wakati na paa za vibanda na meza ni mbovu.

Diwani wa Kata ya Kahama Mjini, Juma Kapama alisema, amekuwa akijenga hoja katika baraza la madiwani juu ya kero hiyo ikiwamo ukarabati wa mitaro ya kupitishia maji sokoni na ukarabati huo unatarajia kufanyika hivi karibu. Baada ya kutembelea soko hilo, mbunge Kishimba aliahidi kufanya maboresho ya miundombinu ya soko hilo kwa kutumia fedha za mfumo wa jimbo na kuchangia mifuko 100 ya saruji ya Sh.milioni 2.2 na kuwataka kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea kutengeneza mazingira rafiki ya biashara.

Alisema mwaka jana alitoa mifuko 70 ya saruji, kokoto na mchanga vikiwa na thamani ya Sh.milioni 2.5 kwa ajili ya kuboresha soko hilo.

Hivyo, aliwataka kuendelea kufanyabiashara kulingana na uwepo wa mazingira yaliyopo, kwamba serikali inaendelea kutatua mahitaji yao na kuhakikisha wanalipa ushuru wa mazao kwa wakati bila kuvutana na maofisa biashara.

Alisema fedha zinazopatikana kutokana na ushuru kiasi kirejea kwao kurekebesha mazingira ya biashara zao.

## RC ataka wafugaji kuuza kuku kupata pesa ya umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewashauri wananchi ambao ni wafugaji kuuza mifugo yao ili waweze kulipia gharama ya kufungiwa umeme na kuondokana na matumizi ya kibatari.

Amesema gharama ya kufungiwa umeme ni Sh. 27,000 gharama ambayo ni sawa na kuuza kuku wawili.

Mndeme alitoa kauli hiyo wakati akizindua programu ya kuwasha umeme katika vijiji 16 kati ya 29 vya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama uliofanyika katika Kijiji cha Kahanga Kata ya Wendele hivi karibu.

Alisema hakutakuwa na ubaguzi wa kufunga umeme kwa wananchi hata kama mtu ana nyumba iliyoezekwa kwa nyasi, kwamba wataunganishiwa nishati bila ubaguzi wowote.

Mndeme alisema kaya ambazo wananchi hawana uwezo wa kumudu gharama ya Sh. 27,000 na wana kuku wauze hata wawili ili kupata kiasi hicho.

Aidha, alimtaka mkandarasi anayesambaza umeme vijijini Tontan Project Ltd kuhakikisha vijiji vyote 146 vinapata umeme ndani ya muda uliopangwa, ili kuwezesha jamii hizo kujiongezea shughuli za uzalishaji kupitia umeme.

"Mkoa ulipokea Sh. bilioni 323 za kusambaza umeme vijijini kati ya hiyo Sh. bilioni 32 zimeletwa Wilaya ya Kahama na jumla ya vijiji 146 vinatakiwa kupata umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka huu, hivyo zile kazi ambazo hazihitaji ujuzi vijana changamkie ili mpate kipato," alisema Mndeme.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani, Diwani wa Kata ya Wendele, Justane Kilunga, alishukuru serikali kwa kutenga fedha na kuhakikisha inasambaza nishati hiyo vijijini kwani wananchi waliokuwa wamekata tamaa ya kupata umeme na huduma nyingine wakijua huduma zote muhimu zinapata mjini tu ila sasa zinafika hadi vijijini.

Akitoa taarifa ya usambazaji wa nishati hiyo, Mhandisi wa mradi wa REA kutoka TANESCO mkoani Shinyanga, Antony Tarimo alisema, wanajukumu la kusambaza nishati wilaya nzima katika vijiji 146 kwa Sh. bilioni 32, kati ya vijiji hivyo 49 vimeshapata umeme na vijiji 97 bado.

Alisema Wilaya ya Ushetu vijiji 17 kati ya 49 vimeshaunganishiwa umeme, Msalala vijiji 16 kati ya 68 vimeshapata umeme, Manispaa ya Kahama vijiji 16 kati ya 29 vimeunganishwa na umeme.

Hivyo, aliahidi kukamilisha vijiji vilivyobaki kwasababu mkandarasi ameongeza muda wa kufanyakazi ili kufidia muda uliopotea na kuwataka wananchi kuacha tabia ya kuiba vifaa hususani nyaya na nguzo.



Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, akiongoza shughuli ya upandaji miti 100 ya kivuli katika chanzo cha maji Mto Kidalu Manispaa ya Shinyanga ili kutunza mazingira. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wakumbushwa kupanda miti kulinda makazi yasibomoke

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI katika Manispaa ya Shinyanga wamekumbushwa kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kupanda miti kwa wingi, ili kutunza mazingira na kulinda makazi yao yasiezuliwe hususani katika vipindi vya mvua za upepo mkali.

Rai hiyo imetolewa jana na Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, wakati wa upandaji miti zaidi ya 100 katika eneo la chanzo cha maji cha Mto wa Kidalu.

Alisema licha ya kuwa na kazi ya kutunza mazingira vilevile ulinzi wa nyumba dhidi ya upepo unaezua paa, hivyo kuwataka wahakikishe wanapanda miti kwa wingi kudhibiti madhara ya namna hiyo kama ilivyotokea hivi karibuni katika baadhi ya maeneo mkoani hapa.

"Nyumba ziliezuliwa na upepo sababu ya kutokuwa na miti, tukipanda miti ya kutosha hayo majanga tutayasahau, pia miti hii tuliyoipanda kwenye chanzo hiki naomba itunzwe na ipate kukua ili kukitunza chanzo chetu kwa maslahi ya vizazi vijavyo," alisema Masumbuko.

Ofisa Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Ezra Manjerenga, alisema upandaji miti ni endelevu na kwamba ndani ya mwaka huu wamepanda miti milioni 1.2 na kwamba maagizo ya serikali ni kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri ndani ya mwaka mzima.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wa Shinyanga kuendelea kupanda miti ya matunda na kivuli na wale ambao wanahitaji miti wanaweza kufika katika ofisi yake ili wapewe bure.

Mwenyekiti wa klabu ya waandishi wa habari mkoani Shinyanga, Greyson Kakuru, akizungumza kwa niaba ya waandishi wa habari ambao wameshiriki upandaji miti, aliipongeza serikali kwa kuendelea kuhamasisha wananchi kutunza mazingira ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

ama
ALHAMISI DESEMBA 28, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

## Kituo Sayansi kimekuja na teknolojia kuzalisha mboga bila kutumia udongo



Ukurasa 13

HALI NA REKODI MBAYA KIMKOA MIMBA, UNAJISI...

## Zimemtia kichefuchefu RPC, ajitosa shule, nyumba za ibada hadi migodini

AHADI YA RAIS & MRADI MAJI ULIKOTOKA ...

# Mwaka 2024 waja na zawadi Bwawa la Nyerere kuihakikishia nchi umeme

**Na Mwandishi Wetu**

FALSAFA yake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kikazi ni 'Kazi Iendelee.' Ina mzizi kwenye ngazi kuu tatu za utumishi wake kwenye Baraza la Mawaziri, akianza Waziri wa Awamu ya Nne ya uongozi wa nchi.

Baadaye Awamu ya Tano, akawa Naibu Mkuu wa Nchi, kwa maana Makamu wa Rais, kabla ya Awamu ya Sita alipokabidhiwa kijiti kuongoza nchi, ndipo akaja na falsafa 'Kazi Iendelee.'

Kwa upekee, Dk. Samia ana suala la kisekta ambalo daima hajawahi kuwa mbali nalo katika utendaji kila siku kiserikali; sekta ya mazingira.

Sehemu mojawapo ya maboresho yake anayoendeleza, ni penye umeme unaoendeshwa na mazingira - maji, ukitarajiwa kumaliza shida ya hitaji hilo kimtaifa.

Ujumbe wake Dk. Samia siku chache zilizopita, ni akijibu malalamiko ya ukatikaji umeme kitaifa, kwamba yatakwisha mwakani, baada ya kuwashwa chungu cha kwanza katika Bwawa la Nyerere mwezi ujao.

Hapo anataja kinu cha kwanza kati ya tisa vya Mwalimu Nyerere, itaanza kufanyika kazi mwezi ujao.

**SAFARI ILIKOTOKEA**

Kinachotekelezwa na Rais Dk. Samia ndani ya falsafa, ina mzizi kuanzia awamu iliyopita kiserikali chini ya Rais Dk. John Magufuli, akiwa na makamu Dk. Samia, ambaye ofisi yake imehusika na mazingira. Mkuu huyo wa nchi kwenye uzinduzi wa mradi umeme wa Julius Nyerere, akatamka:

"Natambua kuwa pamekuwapo na maneno kuwa mradi huu utaharibu mazingira. Lakini, kiukweli mradi huu unayajenga mazingira. Upinzani huo ulianza mara tu tulipotangaza kuanza kutekeleza mradi huu mwezi Juni 2017.

"Hata hivyo, kwa kuwa nchi yetu ni huru na sio maskini, narudia nchi yetu huru na wala siyo maskini kama baadhi ya watu wanavyodhani.

"Tuliamua ni lazima tutekeleze mradi huu, sisi hakuna mtu wa kutufundisha katika suala hili Tanzania. Tanzania ni kinara katika kuhifadhi mazingira."

Hata baada ya kifo chake Rais Dk. Magufuli 'kazi iliendelea' pale January Makamba, Waziri wa Nishati, chini ya Rais Dk. Samia, akawaeleza Watanzania, ujazaji maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), ungeanza Desemba 22 mwaka jana na kushuhudiwa na Rais mwenyewe, leo ikitimu wastani mwaka mmoja na siku tano.

Wakati Makamba anatamka, ilikuwa wiki moja kabla ya tendo hilo, mradi ukiwa umefika asilimia 78 ya utekelezaji tangu kuanza kujengwa. Pia Dk. Samia akautaja tangu anachukua hatamu za kuongoza nchi, ni kati ya miradi mikubwa kitaifa anayoiendeleza, pamoja na reli ya umeme (SGR).

"Tunayo faraja kubwa kwamba, mjadala ambao umekuwa ukiendelea kuhusu dhamira ya serikali kukamilisha mradi huo angalau utaondoka sasa, baada ya kufikia hatua hii (Desemba mwaka jana, asimilia 78).


"Kwa sababu huu ushahidi tosha kwamba, serikali, Rais (Dk. Samia), Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) tumefanya kazi kubwa ya kutekeleza mradi huu kwa nguvu, maarifa na juhudi kwa wakati wote, mahali tulipofika sasa," akanena Makamba, mwaka jana.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wake, Desemba mwaka jana kulishajengwa muundo wa handaki la kuchepusha maji lenye urefu wa mita 700, sawa na viwanja saba vya mpira wa miguu na lilojengwa miaka mitatu kabla kwa gharama ya Sh. bilioni 235.

Ikatajwa, mbali na jukumu la kawaida, bwawa linakuwa kivutio cha watalii, kwa kuwa liko ndani ya hifadhi na taswira mpya.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, akanena inakadiriwa

Inaendelea Uk. 13



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipomsikiliza, Waziri wa Nishati, January Makamba na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Maharage Chande (walipokuwa katika nafasi hizo), kuhusu Kituo cha Kusafirishia Umeme, kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, Desemba mwaka jana, kwenye uzinduzi wa ujazaji maji. **PICHA: MTANDAO.**

MAZINGIRA

ZAMA MPYA, ZENYE NEEMA SHAMBANI...

# Kituo Sayansi kimekuja na teknolojia kuzalisha mboga bila kutumia udongo

**Na Renatha Msungu,** ARUSHA



Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mazao ya Mboga ya Asili ya Kiafrika, ambaye ni Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini wa kituo hicho, Dk. Gabriel Rugalema (katikati), akikagua baadhi ya mazao ya mboga wanayoyafanyia utafiti. **PICHA: MAKTABA**

HADI sasa nchini kuna taasisi ya kimataifa kwa jina la World Vegetable Centre (Worldveg), inayoshughulika na kilimo cha mboga nchini na Afrika, ambayo sasa imekuja na majibu kwa athari za udongo kwenye kilimo.

Aina ya mbadala inayokuja nayo ni kutumia teknolojia mpya na ya kisasa, kuhakikisha wakulima wanainuka kiuchumi, hasa kwenye kilimo hicho cha bustani kuepuka athari za magonjwa kwenye udongo.

Mbinu zilizoanzishwa za kilimo hicho cha udongo, kinajumuisha kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi, pale wanapoanza maandalizi ya kilimo.

Namna kilimo hicho kinavyofanywa ni mimea inapandwa bila ya kutumia udongo, bali kunakuwapo virutubisho vinavyofyonza mizizi kupitia maji ya umwagiliaji.

**UFAFANUZI WA MTAALAMU**

Nickson Mlowe, mtaalamu wa taasisi hiyo anasema, wameamua kuibua teknolojia hiyo rafiki wa mazingira, baada ya kubaini wakulima wengi hupata hasara kubwa, kutokana na magonjwa yanayoathiri mazao shambani.

Anasema, utafiti umethibitisha kuwapo magonjwa mengi ya mimea (mazao) yanayotokana na udongo na wakulima wa mboga nchini, hawako imara kukabili magonjwa hayo.

Mlowe akaeleza kuwa mbinu za kilimo zisizo na udongo, wanatumia mbadala wa miti michafu, akitaja aina zake katika lugha za kitaalamu; Coco peat, Peat Moss na Hydroponics

"Njia hizi ni za maana sana na husaidia wakulima wa mboga kukabiliana na changamoto kadhaa za magonjwa katika mashamba yao, pia wanachukua jukumu muhimu kusaidia wakulima kuhimili athari kali za mabadiliko ya hali ya hewa," anasisitiza.

Mtaalamu Mlowe anafafanua kwamba kituo kitaendelea kufanya utafiti zaidi, kuwahakikishia wakulima wanaojihusisha na sekta muhimu ya uchumi nchini wananufaika ipasavyo kutokana na uwekezaji na juhudi zao za kilimo.

Kwa mujibu wa Mlowe, ni kazi inayofanywa chini ya usimamizi wa Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo ya Mbolea (IFDC), kukiwapo maeneo yaliyotengwa kwa kazi hiyo, Tengeru mkoani Arusha na mji mdogo wa

Soko ulioko chini ya Mlima Meru, zimeundwa kwa ajili ya utafiti na kuanzishwa teknolojia hiyo.

Anasema kituo hicho kinatarajia kuwahudumia zaidi ya wakulima milioni mbili mwaka ujao. Mbali na hiyo, anataja kituo kitajikita katika elimu ya afya ya mchanga, ufanisi wa kutumia maji, mbolea na majaribio ya mbegu hadi kufukia tafsiri pana ya mnyororo wa thamani.

Mlowe anafafanua kuwa, kituo chao kimeshawatambulisha wakulima wa mboga watumia teknolojia, pia kutambua maji kwenye udongo na wamekuwa wakitumia kaulimbiu 'Kupanda Mbegu, Kukutana na Mbegu' Worldveg.'

Anasema, hivi karibuni waliadhimisha miaka 50 ya utendaji wao bora nchini, sasa imezindua majukumu yake mwaka 1992 jijini Arusha.

**MAZAO MBOGA**

Kuhusu mazao ya mboga, Mlowe anataja baadhi kama

nyanya, pilipili, vitunguu na kabichi, pia za mboga za asili Afrika, ikiwa na washirika taasisi zaidi ya 40 za kitaifa na mashirika ya kimataifa.

Anaeleza kuwa kituo kinaendesha vituo vitatu vya kikanda barani Afrika, ikiwamo Tanzania ikiwakilisha Mashariki na Kusini; nchini Mali kwa Afrika Magharibi na Kati, amabako kunatajwa kuwapo ahali ya ukame, mradi ukiwa ulianza mwaka 2014; na Benin, kunakowakilisha Afrika Magharibi na Kati, kukiwakilisa ukanda Pwani, pia wenye unyevu (2017).

Mlowe anaeleza kuna ofisi ya mawasiliano nchini Cameroon, ikisimamia Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa maeneo ya kitaalamu ya aina bora za mboga, pia teknolojia ya uzalishaji.

**NENO LA MKURUGENZI**

Dk. Gabriel Rugalema, Mkurugenzi Mkuu Mshiriki (Afrika) na Mkurugenzi wa Kanda (ESA) katika Kituo cha Mboga cha Dunia (WVC), anasema Tanzania inatarajia kuzindua Benki Kuu ya Vinasaba katika Jiji la Arusha.

Anasema, ni nyenzo itakayosaidia kubaini changamoto zilipo katika sekta hiyo, ikiwamo kuzihifadhi katika uzinduzi unaotarajiwa kufanyika Machi ijayo, ikihudhuria na wadau kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Anasema ni kituo cha mbegu cha kwanza barani Afrika, kitakachochukua jukumu la kuchochea na kuinua utendaji wa jumla wa sekta ya mboga na viungo nchini.

Dk. Gabriel Rugalema, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Mshiriki (Afrika) na Mkurugenzi wa Kanda (ESA) katika Kituo cha Mboga cha Dunia (WVC), anasema benki ya kitaifa ya kisasa, ina vifaa vya kisasa vitavyosaidia kubaini changamoto mbalimbali kilimi tajwa.

"Benki ya Jene tunayojenga ina vifaa vingi muhimu, ikiwa ni pamoja na sehemu maalum za kupokea na kusindika mbegu, mahali pa kukausha mbegu, pamoja na maabara ya mbegu iliyotengenezwa kwa ufundi cherehani," anafafanua Dk. Rugalema.

Lingine Mkurugenzi hiyo analolitaja, ni kwamba kituo kitajumuisha sehemu maalum ya kushughulikia afya ya mbegu.

Anasema pia, kuna uwekaji kituo cha mbegu, Tengeru- mkoani Arusha, akiendeleza ufafanuzi: "Nilipopewa jukumu la kuongoza kituo hiki mwaka 2020, hapakuwa na mradi wowote mkubwa unaohudumia nchi nyingi za Afrika.

"Hivyo, jukumu langu ni kutumikia nchi nyingine, niliamua kuandika pendekezo la mradi mkubwa."

Dk. Rugalema, ama ufafanuzi kwamba wamefanikiwa kupata ufadhili wa Dola za Marekani milioni 6.3, katika nchi nne za Ufalme wa Eswatini, Benin, Madagascar na Tanzania.

Ni mradi anaoutaja nchini unakamilika mwezi huu, ukitarajiwa ukazalisha mboga kwa miaka 99, akisema katika sehemu ya kutekeleza mradi huo nchini, inafanya kazi kwa mwingiliano na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuadudu (TPHPA), kukusanya na kuhifadhi idadi kubwa ya mbegu za mboga, ambazo benki za kaunti zinazitumia.

"Tunafuraha kubwa kwa vile Umoja wa Ulaya (EU) na Udhamini wa Mazao, wamekubali kutufadhili ili kuzindua jumla kitaalamu, tukio hilo zuri ambalo litavutia wadau mbalimbali wa mbegu kutoka ndani na nje ya nchi," alifahamisha.

Dk Rugalema, ambaye hivi karibuni alipandishwa kutoka Mkurugenzi wa WVC kwa Mashariki na Kusini mwa Afrika na kuwa Mkurugenzi Mkuu Mshiriki (Afrika), pia Mkurugenzi Mkuu wa Kanda (ESA), anaishukuru serikali, kufanya nayo kazi kwa karibu.

Anatamka: "Ninasalia na matumaini kwamba serikali katika siku za usoni, itakuwa sehemu ya benki yetu ya Jene, kwani kituo kitachukua jukumu muhimu kuweka hadhi ya mbegu za mboga nchini kwenye jukwaa la kimataifa."

Kituo cha Mboga Duniani (WVC) Genebank kinadumisha mkusanyiko mkubwa zaidi wa wadudu wa mboga duniani na viambatisho 65,152, vilevile takriban mboga 12,000 za kiasili.

Asia Mosha ni mkulima anayesema kituo hicho kimekuwa msaada mkubwa kwa wakulima wa mazao ya bustani, kutokana na kubuni teknolojia mpya katika lengo la kuwakomboa shambani.



Mkurugenzi Dk. Gabriel Rugalema, akikagua moja ya mmea katika kituo hicho. **PICHA; RENATHA MSUNGU.**

AFYA

## HALI NA REKODI MBAYA KIMKOA MIMBA, UNAJISI...

# Zimemtia kichefuchefu RPC, ajitosa shule, nyumba ibada hadi migodini

• Salamu zake, 'ole wake nitakayemnasa!'

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**

MKOA wa Songwe umeshamiri kwa 'uchafu' wa vitendo vya kikatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo ndoa za utotoni, ikitajwa kitakwimu inaongoza kitaifa kwa wastani asilimia 45, kumemtia kichefuchefu, Kamanda wa polisi mkoani Songwe (RPC) Theopista Mallya.

Mwanamama huyo askari, ameamua kujibebesha jukumu, akirejea miongozo yale kikazi, akizunguka kwenye shule, nyumba za ibada na mikusanyiko ya kijamii kutoa elimu namna ya kukabili shida hiyo.

Hiyo ni zao la siku za karibuni, kitakwimu mkoa wa Songwe unatajwa katika sifa hiyo, viongozi wake sasa kwa ngazi zote wakiumiza vichwa kupambana, kuhakikisha wanaondoka kwenye takwimu hiyo 'chafu', lakini Kamanda Mallya kishaanza safari.

Kuna sura inayolalamikiwa kutawala sasa, kuwapo wasichana wenye umri chini ya miaka 18 ama wanaolewa au kuzalishwa badala ya kuwa shule limekuwa ni la kawaida, badala ya kuwapo shule, wilaya za ya Ileje ikiongoza.

Hilo linafanya Kamanda Mallya, anaelekeza nguvu yao kwenye nyumba za ibada, akiwaasa viongozi wa dini na waumini kuungana katika kupinga vitendo vya ukatili na uhalifu, ili mkoa huo ubaki salama.

Ziara za kamanda huo, zikajumuisha makanisani, pia shule anakozungumza na wanafunzi jinsi ya kujikinga au kuepuka ukatili, hasa kukwepa 'vijizawadi' kutoka kwa wanaume wasiowajua.

Baada ya kupita maeneo hayo, pia anaonana na kuzungumza na viongozi wa kimila, ambao baada ya maongezi walikubali kuungana naye kupinga ukatili na uhalifu huo, akikiri kuna ishara ya sura nafuu kampeni inakoelekea.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, akiwa kazini kuelimisha jamii kuhusu ukakasi wa vitendo vya kikatili na unyanyasaji kijinsia. **PICHA : IBRAHIM YASSIN**

Pia moja ya sababu iliyopo kwenye ukatili wa kijinsia, inatoka kwenye familia zenyewe na hata baadhi ya walimu wenye kashfa ya kuwarubuni wanafunzi na kujikuta wanaingia kwenye uhusiano kimapenzi na wanafunzi, hadithi ikiishia kuharibika ndoto zao za kujinafikisha kielimu.

Hivi karibuni akiwa kwenye baadhi ya shule, Kamanda Mallya, akawafafanulia wanafunzi haja ya kuzingatia masomo, waache kujiingiza kwenye yasiyofaa hata kuwaingiza kwenye matatizo, ikiwamo mimba.

Angalizo lake la ukali Kamanda Mallya, ni kwamba polisi haitasita kuchukua hatua kwa watakaobainika kuharibu maisha ya watoto na wale watakaojiingiza, hatua za kisheria akinukuu kibwagizo 'Songwe bila uhalifu na mimba za utotoni inawezekana.'

Kamanda Mallya anaendelea: "Haiwezekani kila siku Songwe isikike kuwa na matukio mabaya, hatutaki kitu kama hicho. Tunataka watu waishi kwa amani, serikali inahangaika kutafuta maendeleo ya wananchi, halafu watu wengine wanataka kurudisha nyuma jitihada hizo!"

**KWA WACHIMBA DHAHABU**

Jitihada za Kamanda Mallya, zimekuwa zinaungwa mkono kila anakopita kwa kuahidiwa 'sapoti'

kukabili uhalifu wa namna hiyo, zikafika hadi kwenye jumuiya ya wachimba dhahabu wadogo.

Hapo akawapa darasa, namna ya kuepuka vitendo vya utumikishaji na kuajiri watoto wadogo kwenye machimbo na jinsi ya kuepuka kujiingiza kwenye uhalifu.

"Hii ni vita ya jamii nzima, kuhakikisha tunaungana kupinga vitendo viovu, ikiwamo mimba, ubakaji, unyang'anyi, ulawiti ndoa za jinsia moja, wizi na kuwaficha watakaobainika kufanya vitendo hivyo, ili sheria ichukue mkondo wake," anasema Kamanda Mallya.

Mzee maarufu mkoani Songwe, anayejulikana kwa jina moja la Mtafya, anamuunga mkono kwa hatua hii iliyoanzishwa na Jeshi la Polisi, ana uhakika Songwe itaondokana na vitendo hivyo vya aibu, kwani takwimu ya kuongoza kitaifa kwa vitendo vya ukatili ni aibu.

Anasema wao wazee, kwa kushirikiana na jamii wakiungana kupinga vitendo hivyo, hasa wazazi wakiwaficha wanaowapa ujauzito wanafunzi kwa kuwapeleka mahakamani, ana imani changamoto hiyo itakwisha.

Mtafya anasema kumekuwapo kawaida ya 'taratibu pori', wazazi wa pande mbili husika wanakutana na kuelewana, wakilipana fedha mbele ya viongozi wa vijiji, wanaowapa mimba wanafunzi, kesi zao hazisongi mahakamani.

Anaiomba serikali kutilia mkazo wa adhabu kwa 'mafataki' wanaowapa ujauzito wanafunzi na kuwachukulia hatua wazazi na viongozi wa vijiji wanaomalizana kwa kukaa mezani kulipana fedha, badala ya kesi kuzipeleka mahakamani, nao wachukuliwe hatua.

Ni aina ya kilio kilichoibuliwa wiki chache kadhaa, kwenye kikao cha uongozi wa mkoa Singida, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, akalalamika kubainika tabia kwa wanafunzi wakiwa wahusika wakuu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo aliyetoa ushahidi wa tabia hizo pia kuonekana tabia hiyo katika wilaya zingine za mkoa, huku kukiwapo ishara kuna watu waliopo nyuma yao kuwaunga mkono, maana watoto hao wakakutwa na vifaa vinavyotumiwa katika unajisi, kama vile ain ya mafuta.

## Mwaka 2024 waja na zawadi Bwawa la Nyerere kuihakikishia nchi umeme

Inatoka Uk. 11

misimu miwili ya kipindi cha mvua, ingeweza kujaza maji katika bwawa hilo.

Bosi huyo wa zamani Tanesco, akafafanua: "Tunaanza kujaza maji mwezi huu wa Desemba ambapo kuna mvua za vuli, pia tunategemea mvua za masika mwezi Machi 2023, ambazo zitakuwa mvua za msimu wa kwanza.

"Pia tutapata vuli ndani ya kipindi hicho, kisha tutapata zile za masika katika mwaka 2024 pamoja na vuli ya kipindi hicho, hivyo mvua mbili kubwa za masika zinaweza kujaza bwawa kwa hesabu zilizopo."

Wakati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuzindua ujazaji maji hayo katika Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), ujenzi wake ulishifika asilimia 78.68.-

Kwenye uzinduzi huo, kikabonyezwa kitufe cha kufunga handaki kuchepusha maji, hivyo kuruhusu kuingia kwenye bwawa la ujazo wa lita bilioni 32, mradi baada ya kukamilika ukirajiwa kuzalisha megawati 2,115 za kukidhi mahitaji kitaifa na ziada, hata kuwa kichocheo cha kuwekeza kimaendeleo nchini.

Kwa mujibu wa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharage Chande, uingizwaji maji unatarajiwa kukamilika mwaka ujao Juni kamili kuanza mwezi Juni.

AFYA

# Kuzagaa kichaa cha mbwa kwa karibisha umauti mama, mtoto; bibi amlilia mjukuu

- Gharama kubwa za chanjo zaleta simanzi
- DC na operesheni kuua mbwa, tayari 70

**Na Neema Emmanuel, aliyekuwa** SENGEREMA

NI zaidi ya huzuni, familia inapopoteza mke na mtoto, huku nyingine bibi akimlilia mjukuu wake. Hofu inatanda kwa wananchi wilayani Sengerema ya kupoteza naisha, kisa mbwa ambao wamegeuka tishio katika eneo hilo.

Ili kunusuru maisha yao wananchi, sasa zaidi ya mbwa 1,000 na paka wawili, wamepatiwa chanjo ya kuwakinga na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Hiyo ni katika kitongoji cha Mabatini, Kata ya Busisi, kukiwapo mikasa ya familia kupoteza wapendwa wao.

Akizungumza na Nipashe, James Jacob (35), baba wa watoto wa tatu aliyepoteza mke na mtoto mtarajiwa, anaeleza kuwa ndoa yake imedumu kwa miaka sita na Agosti 28 mwaka huu furaha ilianza kuyeyuka kutokana na mikasa hiyo.

James anasimulia kuwa, baada ya mkewe kung'atwa na mbwa, baada ya miezi miwili alipoteza mke na mwanawe mtarajiwa, hata ikasambaratika familia, kwani kukalazimika watoto wake watatu waliosalia, kati yao kike wawili wakachukuliwa na mjomba wao, baada ya kuonekana baba hawezi kuwalea. Sasa anabaki mpweke.

**MIKASA ILIVYOKUWA**

Akieleza mkasa wake, James anasema ilitokea majira ya jioni, wakati mkewe aliyekuwa na ujauzito wa miezi saba, alikuwa ametoka kidogo nyumbani na katika safari ya kurejea, ndipo akakutana na mbwa aliyesadikika mwenye kichaa.

James anasimulia mkasa, mbwa alimkimbilia mama huyo na hata yule mama alipojihami kujaribu kukimbia, mbwa alikuwa na kasi zaidi hata akafanikiwa kumng'ata mguuni.

Anasema, siku iliyofuata alimpeleka kuchomwa sindano ya chanjo, ambayo alitakiwa kurejea mara nyingine, lakini kutokana na gharama kuwa juu ya sindano hizo, hakumudu, hivyo virusi vikaendelea kuenea mwilini mwa mkewe hata kumdhuru.

"Gharama za matibabu ni kubwa, kila sindano tulipaswa kulipia Sh. 32,000 na zilitakiwa tano, Sisi hatuna uwezo huo, tulishindwa siku zilivyokuwa zinazidi kwenda, alianza kuumwa nilimpeleka hospitali, huko waliamua kumfanyia upasuaji, ili kunusuru maisha ya mtoto.

"Tulikuwa tumechelewa mtoto alivyotolewa ikaonekana na yeye amepata virusi na baada ya muda alipoteza maisha na siku mbili mke wangu naye akafariki," anafafanua.

James anasema, baada ya mkasa huo, naye alikuwa amefuga mbwa nyumbani kwake, hakutaka tena kusikia neno 'kufuga mbwa', hivyo akawaruhusu waliokuwa wanafanya operesheni ya kuwaua mbwa wasiochanjwa wampige risasi wa kwake.

Hapo anasema akabeba rai wenye mbwa wasiwafiche, bali wawapeleke wapatiwe chanjo, kwa sababu madhara yake ni makubwa.

Pia, katika mkasa wa pili ambao Nipashe ikasimuliwa, ni tukio la muda mfupi baadaye, Bibi Salome Bwire (59), akampoteza mjukuuu wa miaka nane, aliyekuwa anasoma darasa la pili, mwakani akitarajia kuingia la tatu.

Salome anasema katika mkasa wake, siku ya tukio majira ya jioni, mjukuu wake alikuwa kwa nje akicheza na alipomuona babu yake akirejea, akamkimbilia kumpokea, ndipo akakutana na mbwa.



Operesheni ya kuchanja mbwa, ikiendelea kwenye mitaa ya Sengerema Mwanza. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

"Mjukuu wangu alirudi nyuma, lakini mbwa yule alimfuata na kumwangusha chini na kumng'ata maeneo mbalimbali ya mwili, ikiwamo mguuni na mkono.

"Usiku huohuo tulifanikiwa kumchoma sindano ya 'tetenasi' na kesho yake tulimpeleka hospitali kwa ajili ya chanjo, alichoma ya kwanza, baada ya muda tuliambiwa tumpeleke akachome ya pili na tulifanikiwa kuchoma na ya tatu. Ikabaki moja, fedha ikatuishia, tulijua hizo alizopata zitafanya kazi," anaeleza.

Anafafanua kwamba, baada ya muda mtoto huyo akaanza kuumwa na wakampeleka hospitali, ndipo wakapata mrejesho kwamba, hatua aliyofikia alikuwa anapumua kwa shida, anapiga kelele, akigeuka mithili ya mnyama na anatapika damu, hata akapoteza maisha.

**VIONGOZI WA KIJIJI**

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Busisi, Patrick Mussa, anaeleza kuwa hali ni tete dhidi ya kichaa cha mbwa, wananchi wameathirika kiasi kikubwa kutokana na mbwa wanaozagaa mtaani, watu wanapoteza maisha na wengine wakiishi kwa hofu.

"Mimi pia ni mwathirika, mtoto wangu naye ameng'atwa na mbwa Novemba 28 mwaka huu na bado yupo kwenye chanjo. Ametakiwa kuchomwa sindano nne, bado moja.

"Alikuja Mkuu wa Wilaya baada ya kushamiri kwa matukio haya, tuliliongelea hilo akaagiza wataalamu waje wa kuchanja na wengine wa kuwapiga risasi mbwa ambao hawajapelekwa kwenye chanjo.

Pia tulipitisha sheria (agizo) mtu aliyeshindwa kuchanja mbwa wake na akaleta madhara, faini ni laki tano... " anaeleza mwenyekiti huyo.

Anaongeza kuwa uzembe na wananchi kutokuwa makini na mbwa wao na kuzingatia chanjo, ndio chanzo kikuu cha madhara hayo, akiwaomba kila mmoja kuwajibika kuangalia mifugo yake ikiwapo majumbani kwa amani iliyokuwapo awali.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Petro Lubohya, anaeleza kuwa walifanikiwa kuwapiga risasi mbwa wasiokuwa na chanjo 20 na watu takribani 10 waling'atwa wawili, walipoteza maisha, ambao hawakufuata masharti ya chanjo.

Pia anawaagiza wafugaji wanyama hatarishi, kufuata utaratibu wa kuwafunga na kuwapa chanjo na yeyote asiyefuata utaratibu huo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**DAKTARI MIFUGO**

Jerome Said, ni Daktari wa Mifugo Kanda ya Ziwa, anasisitiza mtu yeyote anayepata tatizo hilo, aende hospitali haraka kupata chanjo na asichelewe, kwani muda unavyozidi kwenda ndivyo virusi vinavyosambaa mwili na kufanya kazi.

"Ni muhimu kumaliza chanjo ulizoelekezwa, kwa sababu unapochomwa chanjo ya kwanza ina muda wake wa kufanya kazi, ndipo unatakiwa upate nyingine, ili kuongeza ile kinga, anatamka Dk. Jerome.

Anaendelea: "Tena usiporudia, unaweza ukapata ugonjwa hivyo tunashauri kumaliza chanjo zote ili kupata kinga ya kutosha."

Pia anawasihi wananchi wajitokeze kuchanja mifugo yao na wasisubiri mpaka wanapoleta madhara, kwa sababu gharama za matibabu ni kubwa kuliko kuwachanja.

Kwa mujibu wa Dk. Jerome, gharama za hatua za awali ni kiasi kidogo cha fedha, akitaja wastani kati ya Sh. 1000 na Sh. 2000 na kuna wakati huduma hiyo hutolewa bure.

Pia anasema ni vyema mtu akaenda hospitali moja kwa moja, pale anapokumbwa na shida hiyo, kuliko kukimbilia kwenye maduka ya dawa ambayo hayatoi chanjo ya kichaa cha mbwa.

**WADAU MIFUGO**

Dk. Zacharia Elias ni Mkurugenzi na Mwanzilishi wa shirika linalojihusisha na haki za wanyama Kanda ya Ziwa (LAZAWO), anaeleza kuwa wananchi bado wana uelewa mdogo kwenye masuala ya ufugaji wanyama.

Anataja hilo linachangia kuwapo mwitikio mdogo, hata kukiwapo wito wa kwenda kuchanja mifugo, hivyo elimu pana ya mifugo inahitajika.

Dk. Zacharia anasema, shirika lake linashirikiana na serikali hasa Kanda ya Ziwa na hata baada ya kupata taarifa ya adha za Wanyama kwa wakazi, wa Sengerema, hata zaidi ya mbwa 70 wakauawa kwa kupigwa risasi kwa ufadhili kutoka asasi ya kimataifa Network For Animal (NFA).

Anasema, ikalazimu kwenda kusaidia chanjo na wamefanikiwa kuwafikia mbwa 1000 na paka wawili.

" Ushauri wangu kwa serikali ni kuzitumia sheria za haki za wanyama na magonjwa ya wanyama, ili wananchi waweze kuelewa wanyama wanahitaji kupewa matibabu ikiwamo chanjo. Iwapo ingezingatiwa ipasavyo, majanga hayo yasingekuwepo," anahitimisha.





# Maofisa mifugo Singida wapewa msaada pikipiki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeikabidhi Halmashauri ya Manispaa ya Singida pikipiki tatu kwa ajili ya maofisa mifugo ngazi ya kata, lengo kuu likiwa ni kuboresha utoaji wa huduma za mifugo katika kata zilizopo pembezoni.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, akipokea pikipiki hizo aliwataka maofisa mifugo waliokabidhiwa kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na siyo vinginevyo.

"Ninaamini huduma za mifugo katika kata zenu na kata jirani zitaimarika na wananchi watanufaika kwa elimu ya ufugaji bora pia huduma za dawa za mifugo," alisema.

Pikipiki hizo zimepelekwa katika Kata ya Uhamaka, Mtipa na Mtamaa ambapo pia maofisa hao watatoa huduma kwenye kata jirani baada ya kuwezeshwa vyombo hivyo vya usafiri.

Kiaratu aliwataka maofisa ugani kushirikiana katika kuhakikisha huduma za ugani zote zinaimarika ikiwa ni pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mifugo na kilimo katika kata zao.

Awali, Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida Jeshi Lupembe, alifanya kikao na watumishi ngazi ya kata akihimiza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi shirikishi wa miradi, kubaini vipaumbele vya kata, masuala ya usafi na mazingira, ukusanyaji mapato na kuwakumbusha wajibu wa kila mmoja katika eneo lake la kazi.

"Shirikianeni wote katika kusimamia miradi ya maendeleo, kuainisha vipaumbele vya kata, pia suala la usafi na mazingira na ukusanyaji wa mapato sitakuwa tayari kuwajibishwa kwa ajili ya uzembe wa watu wachache mimi najituma na nyinyi mjitume," alisisitiza.

Hivyo, aliwataka watumishi kuhimiza wananchi kusafisha maeneo kuzunguka nyumba zao na mitaro pamoja na barabara mbele ya nyumba zao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko katika kipindi hiki cha mvua.



Katibu wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamiii Tanzania (SMAUJATA), Kanda ya Ziwa Victoria, Hashim Ramadhan, akitoa elimu kupambana na ukatili wa kijinsia, katika mkutano wa CCM Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi waaswa kubeba jukumu la malezi ya mtoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU wa Ushirika wa Wamama wa Kikrito wa Kanisa Aglikana Tanzania (UMAKI), Magreth Massawa, amewataka wazazi kutimiza wajibu wao wa kushiriki katika malezi na makuzi ya watoto badala ya kuwaachia wasichana wa kazi.

Alitoa wito huo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ibada ya Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma, iliyoandaliwa kwa ajili ya kuliombea taifa na viongozi wake.

Alisema hivi sasa watoto wa kiume wamekuwa katika mazingira hatarishi zaidi ya mtoto wa kike kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu.

Alisema kutokana na hali hiyo wazazi na walezi wanapaswa kutimiza wajibu wao wa kushiriki katika malezi na makuzi ya mtoto ili kuwanusuru katika hali hiyo. "Wazazi wengi hivi sasa tumekuwa bize na mambo ya utafutaji wa maisha hali ambayo inatufanya kushindwa kutimiza wajibu wetu wa malezi na makuzi ya mtoto na kuwaachia wasichana wa kazi au wakaka wa kazi hali ambayo ni hatari kwa ustawi wa watoto wetu," alisema.

Kadhalika, alisema Kanisa la Aglikana Tanzania kupitia UMAKI, wanaompango wa kuanza kutoa mafunzo ya makuzi na malezi ya mtoto kulelewa kiroho na kimwili na kufahamu mahitaji yao. "Mtoto anapaswa kulelewa katika msingi ya kiroho na kimwili ili atambue haki zake za msingi ikiwamo kupata elimu na kulindwa na vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia.

"Lakini katika mafunzo hayo tunapanga kuelimisha wazazi umuhimu wa zile siku 1,000 za makuzi ya mtoto tangu mimba inapotungwa kwani pale ndipo mzazi akikosea anamuharibu mtoto kabisa," alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kuilinda amani iliyopo nchini na kuliombea taifa na viongozi wake.

Alisema: "Amani kuipoteza ni jambo jepesi sana lakini kuirudisha ni kazi sana, hivyo Watanzania hawana budi kuendelea kuilinda kwa hali na mali ili iendele kudumu kama ambavyo iliasisiwa na viongozi wetu waliotangulia".

## Wanafunzi wenye ulemavu wapewa msaada bima ya afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Wezesha Wanawake mkoani Singida limetoa msaada wa vifaa pamoja na bima ya afya kwa wanafunzi wenye ulemavu ikiwa ni mkakati wa kuwapa faraja watu wenye mahitaji maalumu.

Vifaa vilivyotolewa na shirika hilo ni pamoja baiskeli za walemavu tano, vyakula na vinywaji na bima kwa wanafunzi wote wanaosoma katika shule za walemavu zilizopo katika Manispaa ya Singida vikiwa na thamani ya Sh.milioni saba.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Happy Francis, akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vitu hivyo, alisema mipango yao kwa mwaka 2025 ni kusaidia na kuwapa watu wenye mahitaji maalumu Faraja.

Francis alisema kuwa bima hizo zinapatikana kwa kushirikiana na baadhi ya wadau ambao wameshiriki katika tukio hilo kwa nguvu kubwa kutoka kwao kwa kuanzisha wazo hilo, huku akiweka wazi kuwa watoto wenye ulemavu wanakosa uhakika wa matibabu, ndiyo sababu ya kuweza kujikita zaidi katika bima.

"Sisi tumeona kabisa kwamba watoto wanakosa uhakika wa matibabu, hivyo tumeona tuwekeze katika bima pindi watakapopata magonjwa wapate kutibiwa na kupitia hafla hii watapata bima watoto yenye thamani ya shilingi milioni saba," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, katika hafla ya kukabidhi kadi za bima alichangia Sh.150,000 kwa ajili ya watoto hao ambao wanamahitaji maalumu.

Wadau wengine walichangia misaada mbalimbali ikiwamo Benki ya NBC, viongozi wa dini pamoja na wadau ili kufanikisha lengo hilo maalumu kwa ajili ya watoto wenye ulemavu.

Katika hatua nyingine madiwani mkoani Singida wametakiwa kufanyakazi kwa bidiii kwa kuwahudumia wananchi wanaowaongoza katika maeneo yao kama ambayo walivyokuwa wanaomba kura kipindi cha kampeni ya kuwahudumia na kuwatatulia kero zao za maendeleo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata, akizungumza jana alisema wananchi wa Singida hawana tegemeo lingine katika kuwaletea maendeleo zaidi ya madiwani hao kuchapa kazi kwa bidiii na ndiyo maana wamewapa dhamana ya uongozi.

Mlata alitaja baadhi ya maendeleo ambayo yanaweza yakaletwa na viongozi hao ni pamoja na miundombinu, mazingira mazuri katika kilimo pamoja na upatikanaji wa maji safi na salama.





Wananchi wa Jimbo la Kavuu, Halmashauri ya Mpimbwe wakijumuika kwenye hafla maalum ya chakula iliyoandaliwa na Mbunge wao ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Geophrey Pinda, kusherehekea Sikukuu ya Krismasi juzi. Hafla hiyo imefanyika nyumbani kwake Kibaoni mkoani Katavi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wazazi wakiri kuwashawishi watoto kufeli mitihani

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa Kijiji cha Nyeregete kilichopo katika Kata ya Rujewa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamekiri kuwa walikuwa wanawashawishi watoto wao kufanya vibaya kwenye mitihani ya darasa la saba ili wasifaulu.

Wananchi hao wamesema walikuwa wanafanya hivyo kwa kuhofia watoto wao kupangiwa shule za sekondari za mbali kutokana na eneo hilo kutokuwa na shule ya sekondari.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa Shule ya Sekondari Nyeregete wananchi hao walisema watoto wao waliokuwa wanafaulu darasa la saba walikuwa wanapangiwa kwenda kusoma Shule ya Sekondari Rujewa.

Adelina Filijumile alisema kutoka katika eneo lao kwenda katika Shule ya Sekondari Rujewa kuna umbali wa zaidi ya kilomita 15 hali iliyokuwa inawalazimu kuwatafutia watoto wao nyumba za kuishi.

Alisema kutokana na hali hiyo baadhi ya wanafunzi waliopangiwa kusoma shule hiyo walikatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito na wengine kuamua kuacha shule kutokana na ugumu wa maisha.

Alisema hali hiyo ilikuwa inawakatisha tamaa baadhi ya wazazi na hivyo kuamua kuwashawishi watoto wao kutofanya vizuri mitihani ya darasa la saba.

"Changamoto ilikuwa kubwa kutokana na umbali wa shule, wanafunzi wakifaulu darasa la saba wazazi walilazimika kuwapangishia nyumba jirani na shule ambako huko walikosa ulinzi na kujiingiza kwenye matendo yasiyofaa," alisema Adelina.

Alisema baadhi ya wazazi walikuwa hawaoni haja ya watoto wao kusoma na kwamba wengine walikuwa wanawaficha watoto waliofaulu ili wasiende sekondari.

Naye Sifa Njahali alisema ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyeregete utawasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwenye shule za msingi zilizopo kwenye kata hiyo. Vilevile alisema itasaidia kupunguza gharama ambazo wazazi walikuwa wanalazimika kuwatafutia nyumba za kupanga watoto hao karibu na Shule ya Sekondari Rujewa ambako pia kulikuwa na matatizo mengi.

Hata hivyo alisema itasaidia kupunguza mimba za utotoni kwa maelezo kuwa watoto wakisoma jirani hata kuwalinda inakuwa rahisi tofauti na wanapoishi peke yao mbali na nyumbani.

"Lakini hata watoto wa kiume ambao wamekuwa wakijiingiza kwenye makundi yasiyofaa ikiwamo kuvuta bangi, wataacha kwa sababu tutakuwa tunawalinda kirahisi," alisema Sifa.

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Mbarali, Tuntufye Chamba, aliwataka wazazi kuwa na mwamko wa kuwapeleka watoto wao shuleni kutokana na serikali kuendelea kuboresha mazingira ya elimu.

Alisema kitendo cha serikali kujenga sekondari karibu na maeneo yao lengo ni kuwasogezea huduma za kijamii na hivyo akawataka kuwa na mwitikio chanya kwa maelezo kuwa kwa sasa hakuna malipo ya ada.

Alisema ujenzi wa shule hiyo umezingatia mahitaji muhimu yote ya kielimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya maabara kwa ajili ya masomo ya vitendo kwa wanafunzi pamoja na vifaa vyote vya kielimu.

Ofisa Mipango wa Wilaya ya Mbarali, Salifu Venance, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutunza miundombinu ya shule hiyo ambayo imegharimu zaidi ya Sh. milioni 500 ili idumu na kutumika muda mrefu kwa vizazi vya sasa na baadaye.

# Polisi yatuma salamu madereva wanaochezea 'mfumo'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa baadhi ya madereva wa mabasi nchini wamekuwa wakichezea vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari ili wasionekane, hali ambayo inawafanya waendeshe kwa mwendokasi na kusababisha ajali.

Mwanasheria wa Kikosi cha Polisi Usalama Barabarani, Mrakibu Mwandamini wa Polisi, Deus Sokoni, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipoongoza wadau mbalimbali wa usalama barabaani kukagua mabasi.

Aliwataka madereva kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa wakibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwamo kupelekwa mahakamani na kufungiwa leseni zao ili wasifanye kazi hiyo.

"Mimi mwenyewe nimeshuhudia kwenye baadhi ya maeneo madereva wakifanya uhuni huo, unakuta gari haionekani kwenye mfumo lakini linakamatwa na 'trafic' kwa kosa la mwendokasi," alisema Sokoni.

Aliwataka wamiliki wa mabasi kuhakikisha wanawaelimisha madereva wao ili kuepuka kukumbana na adhabu kwa maelezo kuwa baadhi ya wamiliki ndio wamekuwa wakiwachochea madereva kufanya uhuni huo.

# Idadi watalii wanaokwenda Ziwa Nyasa yaongezeka

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SIKU chacha baada ya Bodi ya Utalii (TTB) kuanza kuhamasisha utalii katika fukwe za Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, idadi ya watalii wa ndani imeanza kuongezeka kwa kasi.

Hivi karibuni TTB ilianza utekelezaji wa Mradi maalumu wa Kukuza Utalii Kusini (REGROW) ambapo maofisa wa bodi hiyo walitembelea maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa lengo la kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii.

Moja ya vivutio ambavyo maofisa hao walitembelea ni fukwe za Ziwa Nyasa hasa Matema, utalii wa utamaduni hasa ngoma za asili pamoja, Ziwa Ngosi pamoja na maporomoko ya Kalambo mkoani Rukwa.

Juzi zaidi ya watalii wa ndani 600 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya, walitembelea fukwe ya Matema kwa ajili ya kupumzika, kujifunza vitu mbalimbali pamoja na kufanya mikutano ya kufunga mwaka.

Watalii hao waliunganishwa na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Naibu Waziri Mahundi, alisema aliamua kuandaa ziara hiyo kwa lengo la kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan na Filamu ya The Royal Tour ambayo inalenga kuhamasisha utalii wa ndani.

Alisema watalii wengi hasa wa kigeni wamekuwa wakikimbilia katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambako kuna hifadhi nyingi za wanyama na kwamba kwa sasa serikali imeanza kuhamasisha usawa wa utalii katika kanda zote.

"Hili eneo ni zuri sana, hapa mimi niliamua kuja na kundi hili la wanawake kwa lengo la kufanya mikutano yetu ya kufungia mwaka, wengi walikuwa hawajawahi kufika eneo hili lakini leo wamefika na wamefurahia," alisema Mahundi.

Alisema mbali na vikao walivyofanya lakini wanawake hao waliogelea na kufurahia mazingira ya fukwe hizo ambazo zina mchanga safi.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, alimpongeza Naibu Waziri Mahundi kwa kuamua kuwapeleka watalii hao katika eneo hilo kwa maelezo kuwa itawajengea utamaduni wa kutembelea maeneo hayo mara kwa mara.

Alisema katika ufukwe huo kuna vivutio vingi vya watalii ikiwemo samaki wa mapambo ambao hawapatikani katika eneo lingine lolote duniani.

Vilevile alisema kuna utalii wa kiutamaduni wa vyungu vinavyotengenezwa na wakazi wa eneo la Ikombe pamoja na ngoma mbalimbali za asili.

"Tunawakaribisha pia wawekezaji kuja kuwekeza kwenye eneo hili, tunawakaribisha wawekezaji wa kujenga hoteli, kujenga viwanda vya kusindika dagaa na samaki ambao wanapatikana kwa wingi kwenye eneo hili," alisema Josephine.

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Rungwe, Amon Sauli ambaye ni miongoni mwa wawekezaji kwenye eneo hilo alisema kwa sasa watalii wamekuwa wakiongezeka kwa kasi kutokana na uwekezaji unaofanyika.

Alisema mbali na vivutio vilivyopo ndani ya ziwa hilo pamoja na fukwe zake pia ni rahisi watalii kufurahia kwa kuona safu za milima ya Livingston.





# Idadi ya watalii walioingia Zanzibar Novemba yapaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wageni walioingia visiwani Zanzibar kwa kipindi cha Novemba mwaka huu imeongezeka na kufikia 57,296, ikilinganishwa na Oktoba ambao walikuwa 54,961.

Mkuu wa Divisheni ya Takwimu za utoaji huduma kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakari Khamis Kondo, alisema wageni 42,488 wanatoka Ulaya sawa na asilimia 74.2 ya wageni wote wa kipindi cha Novemba. "Bara la Ulaya ndiyo linaloongoza kwa kuwa na wageni wengi waliofika nchini, likifuatiwa na Bara la Afrika ambalo lilikuwa na wageni 6,646 sawa na asilimia 11.6 ya wageni wote," alisema Kondo.

Mkuu huyo alisema Bara la Amerika ni la tatu kwa kuwa na wageni 5,353 sawa na asilimia 9.3 na Bara la Asia lilikuwa na wageni 460 ambao ni chini ya asilimia 0.8.

Aidha alisema nchi tano zilizoongoza kwa kuleta wageni wengi ni Italia ambayo ilikuwa na wageni 6,590 sawa na asilimia 11.5, ikifuatiwa na Poland ilikuwa na wageni 6,148 sawa na asilimia 10.7 na Ufaransa ikiwa na wageni 5,226 sawa na asilimia 9.1.

Alisema Ujerumani ilikuwa na wageni 4,765 sawa na asilima 8.3 na Marekani ilikuwa na wageni 3,990 sawa na asilimia 7.0.

Hata hivyo alisema asilimia 86.2 sawa na wageni 49,414 waliingia nchini kupitia usafiri wa anga kupitia katika viwanja vya ndege vya Abeid Amani Karume na asilimia 13.8 sawa na wageni 7,882 waliingia kwa kupitia Bandari ya Malindi Unguja. Pia alisema wageni wote walioingia nchini ni 30,411 ni wanaume sawa na asilima 53.1 na wageni 26,885 wanawake sawa na asilimia 46.9, ambapo asilimia 9.5 ni wageni wenye umri kati ya miaka 65, asilimia 4.0 wenye umri wa miaka 15 na asilimia 86 ni wenyeumri wa miaka 15 hadi 64.

Akizungumzia madhumuni ya wageni hao kuingia nchini, Kondo alisema wengi wao wamefika kwa mapumziko ambao ni asilimia 95.6, asilimia 0.4 kwa ajili ya kuwatembelea ndugu na marafiki na asilimia 4.0 ni kwa ajili ya sababu zingine ikiwamo za mafunzo.

Alisema wastani wa siku walizokaa wageni hao ni wiki moja ambapo asilimia 74.5 walikaa kwa siku moja hadi tisa na asilimia 25.4 walikaa siku 10 na zaidi.

Akitaja uingiaji wa wageni kwa muda wa miaka mitano alisema mwaka 2019 wageni walioingia ni 538,264, mwaka 2020 ni 260,644, mwaka 2021 walikuwa 394,185, mwaka 2022 walikuwa 548,503 na mwaka 2023 walikuwa 568,312.

Meneja Uchumi wa Benki Kuu Tanzania Ofisi ya Zanzibar, Moto Ng'wingande, alisema kuongezeka kwa idadi hiyo ya watalii kunaashiria kukua kwa uchumi wa Zanzibar na wananchi kunufaika kutokana na sekta ya utalii.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah (wa pili kulia), akifungua pazia kuashiria uzinduzi wa uwekaji jiwe la msingi la Soko la Mwanyanya Wilaya ya Magharib A, Unguja, ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za Miaka 60 ya Mapinduzi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajinasibu utoaji huduma bora kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali itaendelea kuwapatia huduma bora wananchi kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na miongozo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo na mafanikio ya wizara katika miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali imeimarisha mbinu za utendaji kazi ili kutoa huduma kwa haraka na zilizo bora kwa jamii kwa kuzingatia utawala wa sheria na haki za binadamu.

Aidha, alisema sekta ya sheria imepewa jukumu la kusimamia masuala ya kisheria ili kuhakikisha Zanzibar inazingatia utawala wa sheria na haki za binadamu.

Waziri huyo alisema serikali itaendelea kusimamia utoaji wa haki na kufanya mapitio ya sheria mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Alisema serikali imefanya juhudi kubwa katika kuanzisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya utoaji huduma ikiwamo ya mishahara, manunuzi, ajira, ukaguzi uwekaji wa taarifa za watumishi na malipo yao pamoja mfumo wa ofisi mtandao. Waziri Haroun alisema Wizara ya Utumishi imekuwa na mikakati endelevu ya kuwajengea mazingira mazuri watumishi wa umma pamoja na kuimarisha maslahi yao.

Hata hivyo alisema serikali imeimarisha Mahakama kwa kuongeza idadi ya majaji, mahakimu na watendaji mbalimbali kwa kurahisisha uendeshaji wa kesi na utoaji wa haki kwa wananchi.

# UVCCM kufanya matembezi kuenzi Mapinduzi ya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) unatarajia kufanya matembezi ya hiari.

Matembezi hayo yatazinduliwa leo na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Miwnyi katika Uwanja wa Makopeni mkoani Pemba.

Matembezi hayo yatafanyika kwa muda wa siku 15, yatafungwa Januari 10 na Rais Samia Suluhu katika viwanja ya Maisara Mjini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM, Mussa Haji Mussa, alisema katika matembezi hayo yatashirikisha vijana 1,000 kutoka mikoa yote ya Tanzania na watatembea kwa kutekeleza na kuenzi falsafa mbalimbali za waasisi wa mapinduzi akiwamo Hayati Abeid Amani Karume.

Alisema vijana hao watatembea kilomita 251 kwa wilaya zote za Unguja na Pemba lakini harakati hizo za matembezi zitaambatana na shughuli za ujenzi wa taifa ikiwamo uzinduzi wa miradi, uwekaji wa mawe ya msingi.

"Matembezi haya yatakuwa na malengo makubwa matatu ikiwamo kuunga mkono na kuezi kifikra na vitendo Mapinduzi ya Zanzibar, kutangaza na kuhamasisha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2025 na kuendelea kuwaunganisha vijana wa nchi nzima kubadilishana mawazo kuhusu maslahi mapana ya taifa letu," alisema.

Aidha, alisema vijana wa CCM watatembelea wilaya zote za kichama, huku wakihamasisha na kutangaza hatua kubwa za maendeleo zilizofikiwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020/2025.

Alisema pia watahamasisha vijana na wananchi kuendelea kujitokeza katika kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na maandalizi ya kufanikisha ushindi wa chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Alisema amani na utulivu iliopo Zanzibar inatoa fursa pana kwa wananchi kuendelea kufanya shughuli za kujiingizia kipato na kukuza uchumi wao.

"Katika eneo hili la uimarishaji wa amani na utulivu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanikiwa na imefanya kazi kubwa sana, na hali ya amani, umoja na mshikamano ni wa hali ya juu sana," alisema.

Hata hivyo alisema UVCCM imebaini kuna baadhi ya watu pengine kwa kutaka umaarufu, kutaka madaraka au kukusudia kukwamisha juhudi za serikali kwa kufanya mambo na kutamka kauli za kuashiria kuvunja amani na utulivu uliopo.

Alisema vitendo hivyo vinadhamira ya kudhoofisha malengo ya mapinduzi, hivyo UVCCM haitovumilia na watashikamana katika kupambana na watu hao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**AISHA HAMISI RASHID** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 14433-0001** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI BALILI mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/52236/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JOHN KASTABU KITALI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **PIAGO** yenye usajili namba **MC 834 CBJ,** CHASSIS NAMBA: ***MBX0002CFWJ712196*** na ENGINE NAMBA: **TBPDMHW3013283.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KW/RB/1280/2022**

## TANGAZO.

Tunatangazia umma kuwa tunafunga kampuni yetu yenye jina la **UKM MICROFINANCE COMPANY LIMITED** yenye namba za usajili 141040588 iliyopo Morogoro mjini, eneo la soko kuu Chifu Kingalu, kuanzia tarehe 18/12/2023.

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT**
**AT KIKUYU**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.27432/2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ALEXANDER DAVID MWAKITALU**

**AND**

**ELIAH ALEXANDER....................................APPLICANT**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 26th day of JANUARY, 2024.

Dated at Rungwe this 13th day of DECEMBER, 2023

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27100/2023**

**In the matter of the Estate of the late ALPHA MUISA TUPA of Nzuguni within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY HAPPYNES MSANJILA NGHAMBI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of January, 2024
Dated at Dodoma this 6thDay of December, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

## TANGAZO LA NOTISI KULIPA DENI

Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd, tunatangaza notisi ya siku kumi na nne na thelathini (30) tangu tarehe ya tangazo hili gazetini kwa wadaiwa sugu waliokopa na kushindwa kulipa madeni ya mkopo yao kulingana na makubaliano ya mkataba.

Wanatakiwa kulipa madeni yao yote ndani ya muda uliotajwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:-

| Mdaiwa/ mdhamini | Aina ya Notisi | Mahali Anapoishi |
|---|---|---|
| Shafii Zidadu Salim Mkwepu | Siku kumi na nne (14 days) | Kata ya Kisarawe II, Mtaa wa Kigogo. Kigamboni - DSM |
| Peter James Stima/ Rehema Ahmad Salum (Mkopaji) | Siku thelathini (30 days) | Ukonga Madafu- ILALA - DSM |

Notisi hizi zitatumika kuanzia tarehe ya tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yenu endapo mtashindwa kulipa madeni ya mikopo yenu ndani ya muda ulioainishwa kwenye tangazo hili. Hii itakuwa ni pamoja na kukamata na kuuza mali zilizotumika kudhamini mikopo mliochukua

**Mawasiliano piga:**
**+255 222774742/ 0677045064/0677045057**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wapalestina 241 wauawa kwenye shambulizi Gaza

**GAZA,** PALESTINA

WIZARA ya Afya chini ya serikali ya Hamas, inayotawala Ukanda wa Gaza, imesema watu 241 waliuawa katika mashambulizi yaliyofanywa na majeshi ya Israel ndani ya saa 24 zilizopita.

Aidha, Rais wa Palestina, Mahmoud Abbas, ametaja vita hivyo ni uhalifu mkubwa dhidi ya wananchi wake.

Katika taarifa ya Mkuu wa Jeshi la Israel, Herzi Halevi ilisema mapigano hayo yataendelea kwa miezi mingi zaidi. Alisema Israel ilipiga zaidi ya maeneo 100 Jumanne, na kusisitiza operesheni za ardhini zinakaribia katikati mwa Gaza.

Wakati huo huo, milipuko mikubwa ilisikika katika eneo la Ukanda wa Gaza jirani na Israel asubuhi ya jana.

Wizara ya Afya ya Gaza ilisema watu 382 walijeruhiwa katika muda wa saa 24 zilizopita.

Kulingana na wizara hiyo, Wapalestina wasiopungua 20,915 wameuawa, miongoni mwao wakiwa watoto na wanawake tangu kuanza kwa vita hiyo.

Watu wapatao 1,200, hasa raia, waliuawa. Takribani watu 240 walirudishwa Gaza kama mateka na baadhi yao waliachiliwa baadaye.

Siku chache zilizopita, Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu alionya kwamba kile anachokiita kuwa operesheni haijakaribia kuisha Ukanda wa Gaza.

Juliette Touma, ambaye ni msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNWRA) aliiambia BBC kuwa kuna ripoti ya kutisha katika maeneo mbalimbali ya Gaza.

"Tunaona ripoti za kutisha sana za baa la njaa katika baadhi ya maeneo, vita vinaendelea vinasababisha uhamisho usio halali na pia makazi ya Umoja wa Mataifa yamezidiwa na idadi kubwa ya watu waliokimbia makazi yao." Alisema Touma.

Israel imetoa tahadhari kwa raia wake nchini India baada ya mlipuko karibu na ubalozi wa nchi hiyo huko Delhi.

Mlipuko huo ulifanyika Jumanne jioni katika eneo la kidiplomasia la mji mkuu wa Chanakyapuri.

Hakuna mtu aliyejeruhiwa, lakini polisi walisema walipata vipande kutoka mahali hapo. Uchunguzi unaendelea.

Aidha, Jeshi la Israel iliwaonya raia wake wanaoishi nchini India kuepuka kwenda katika maeneo yenye watu wengi kama vile maduka makubwa na masoko kwa kuhofia usalama wao.

Tahadhari imetolewa baada ya kutokea mlipuko nje ya jengo la ubalozi wa nchi hiyo ulioko nchini India jana.

Katika ujumbe uliotolewa na Makao Makuu ya Usalama wa Taifa (NSH), iliwaonya Waisraeli wanaokaa India hasa mjini Delhi kuwa makini na waepuke kuonyesha ishara za Israel hadharani na wasichapishe maelezo ya safari au picha zao kwenye mitandao ya kijamii.

Mapema mwezi huu, NSH ilionya Waisraeli kufikiria upya safari zao zote nje ya nchi na kutoa wito kwa wale wanaohitaji kusafiri ng'ambo kuepuka utambulisho wao wa Kiyahudi wakati wa vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza. **BBC**

## Nawaz Sharif kuwania uwaziri mkuu Pakistan

**ISLAMABAD,** PAKISTAN

CHAMA kinachoongozwa na Waziri Mkuu wa zamani wa Pakistan, Nawaz Sharif, kimesema kiongozi wake atawania nafasi hiyo kwa kipindi cha nne.

Katika taarifa yake kilisisitiza kwamba Sharif atakuwa mgombea wake katika uchaguzi ujao wa bunge.

Oktoba mwaka huu, Sharif alirudi Pakistan baada ya kukaa uhamishoni nchini Uingereza kwa miaka minne ili kuepuka kutumikia kifungo chake kwa makosa ya ufisadi.





Viongozi wa upinzani Martin Fayulu (kulia), Theodore Ngoy na Denis Mukwege (kushoto), wakiwa katika mkutano na waandishi wa habari kupinga matokeo ya uchaguzi yanayoendelea kutolewa na Tume ya Uchaguzi jana. **PICHA: DW**

# Upinzani DRC waitisha maandamano

**KIMSHASA,** DRC

WAKATI matokeo ya urais yanaendelea kutolewa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wagombea wa vyama vya upinzani wameitisha maandamano nchi nzima wakishinikiza kurudiwa kwa uchaguzi mkuu.

Zoezi la upigaji kura katika nafasi mbalimbali nchini humo lilifanyika kwa siku mbili kuanzia Desemba 20, lakini lilitawaliwa na vurugu na malalamiko ya kuwepo kwa vitendo vya ukuikwaji wa katiba.

Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali linaloitwa Filimbi, Mino Bompomi, alisema mchaguzi huo lazima urudiwa kwa sababu unakwenda kinyume na sheria za nchi hiyo.

Baadhi ya viongozi wa kambi ya upinzani waliitisha maandamano ya nchi nzima wakidai uchaguzi huo ni bandia.

Wagombea hao, Martin Fayulu, Denis Mukwege na Théodore Ngoy wamepinga pia hatua ya kuongezwa muda wa ziada wakati wa zoezi la upigaji kura.

Ngoy ambaye ni msemaji wa wagombea watano alisema hawautambui uchaguzi huo na matokeo yanayotangazwa na tume ya uchaguzi ni batili.

"Wananchi wa DRC ni mashahidi na waathirika wa kasoro za wazi za uchaguzi bandia uliofanywa na Tume ya Uchaguzi (CENI), watakuwa mitaani leo (jana), kupinga mapinduzi ya uchaguzi yanayoandaliwa na mwenyekiti wa tume," alisema Ngoy.

Kambi ya upinzani ambayo iligawanyika wakati wa uchaguzi mkuu, waliamua kuungana kwa kushirikiana kupinga matokeo ya uchaguzi huo kupitia maandamano.

Wanachama mbalimbali wa upinzani wamethibitisha kuwa majadiliano yanaendelea na kwamba maandamano ya pamoja yanaweza kupangwa katika siku zinazokuja.

Chama cha Ensemble pour la République, ambacho mgombea wake wa urais ni Moise Katumbi, kimeapa kwamba kuungana na vyama vingine ili kulazimisha uchaguzi urudiwe.

Rais anayewania muhula wa pili, Felix Tshisekedi, anaendelea kuongoza kwenye matokeo ya awali kwa kupata kura asilimia 74, akifuatiwa na Moise Katumbi ambaye amepata asilimia 14 na watatu ni Martin Fayulu aliyepata kura asilimia nne.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Ndani, Peter Kazadi, alipiga marufuku maandamano hayo akieleza yanalenga kuvuruga mchakato wa kuhesabu kura.

Serikali imewatawanya maelfu ya polisi na wanajeshi kwenye mji wa Lubumbashi ambayo ni ngome ya Katumbi, ikielezea hatua hiyo ni kuzuia vitendo vya vurugu.

Enoch Kavindele, ambaye ni kiongozi wa ujumbe wa waangalizi wa jumuiya ya nchi za kusini mwa Afrika, (SADC), alisema wanasubiri kuona mchakato wa kuhesabu kura unakamilika kwa amani.

"Hatuna ushahidi kuhusu hilo, sisi kama watu wengine pia tunasubiri na tunaamini kama tume ya uchaguzi itafanya kazi nzuri. Kwa nini ikubali matokeo ambayo haiendani na matakwa ya watu," alisema Kavindele.

**DW**

# YANGA, SINGIDA ZAGONGANA KWA BOLA

**Na Saada Akida**

IKIWA siku 17 zimepita tangu kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili, klabu ya Yanga na Singida Fountain Gate FC zimeingia kwenye vita vya kuwania saini ya mshambuliaji wa Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Emmanuel Bola.

Timu hizo zote zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji huyo mwenye uwezo mkubwa wa kufumania nyavu.

Kwa mujibu wa chanzo cha habari kinaeleza kuwa uongozi wa Singida Fountain Gate FC upo kiwenye mkakati wa kukiimarisha kikosi chao na tayari wameanza mazungumzo na nyota huyo.

"Bola alikuwa akitakiwa na Yanga lakini sasa Singida Fountain Gate FC wameingilia kati wanamtaka mchezaji huyo na ninachofahamu mazungumzo yanaendelea," alisema mmoja wa viongozi wa Singida.

Hata hivyo alisema suala ambalo linaweza kukwamisha mchakato huo ni adhabu waliyopewa Singida Fountain Gate na Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA) la kutosajili.

Nipashe lilimtafuta msemaji wa timu hiyo, Hussein Massanza ambaye alisema suala la usajili kwa sasa hawawezi kuliweka wazi kwa kuwa wako kwenye adhabu ya Fifa.

"Kwa sasa tupo kwenye mchakato wa kumalizana na adhabu tuliyopewa kwa kuwalipa wanaotudai na baada ya hapo tunaweza tukawa kwenye nafasi nzuri ya kusajili," alisema Massanza.

Alisema wanaimani watafutiwa adhabu hiyo kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa kwa sababu viongozi wanaendelea na mchakato wa kukamilisha malipo ya aliyekuwa mchezaji wao Pascal Wawa.



Kikosi cha Bubombi FC kinachotarajiwa kushuka katika Uwanja wa Maji Shirati Sota kuvaana na Kabwana FC kusaka nafasi ya mshindi wa tatu wa michuano ya Umoja Cup Rorya 2023. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bingwa Umoja Cup 2023 Rorya kujulikana Jumapili

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

BINGWA wa michuano ya Umoja Cup 2023 wilayani Rorya anatarajiwa kujulikana Jumapili wiki hii katika mchezo wa fainali utakaopigwa Uwanja wa Maji Shirati Sota kati ya wenyeji wa mashindano hayo, Wanamaji FC na Shirati Mji FC.

Wanamaji FC wametinga fainali baada ya kuwachapa Vijana wa Mpakani Bubombi FC kwa bao 1-0 katika mchezo wa nusu fainali uliokuwa mgumu na wa kuvutia.

Goli pekee la mchezo huo lilipatikana katika dakika ya 70 ya mchezo kwa shuti kali baada ya kutokea piga ni kupige katika lango la Bubombi FC.

Katika kipindi cha kwanza Wanamaji walikuwa wakifika eneo la hatari la Bubombi FC, lakini mabeki wa Bubombi wakiongozwa na nahodha wao, Decko walikaa vizuri kumlinda golikipa wao, Simon Simon.

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya mechi hiyo, Mwenyekiti wa Wanamaji FC, Jofrey Wagara, alisema kazi yake ya kwanza ni kuhakikisha Kombe la Umoja Rorya mwaka huu linabaki Sota kwa kuifunga Shirati Mji FC ambayo ilikuwa ya kwanza kutangulia fainali baada ya kuitupa nje Kabwana FC.

Wagara ambaye alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Wanamaji mwanzoni mwa mwaka huu, alisema mashindano hayo ya Umoja Cup yamewapa nafasi nzuri kipindi hiki wakijiandaa kwa usajili wa Ligi Daraja la Tatu ngazi ya Mkoa wa Mara ambapo Wanamaji na Shirati Mji zitawakilisha Wilaya ya Rorya.

Tayari Ofisa Michezo wa Mkoa wa Mara, Makondo Makondo, ambaye atakuwa mgeni rasmi katika mchezo huo wa fainali, amethibitisha uwepo wake Jumapili kwenye mtanange huo unaotarajiwa kuwa mkali na wakuvutia.

Kabla ya mchezo huo wa fainali Jumapili, Jumamosi kutapigwa mechi nyingine ya kutafuta mshindi wa tatu kati ya Kabwana FC na Vijana wa Mpakani, Bubombi FC.

Katika michuano hiyo inayodhaminiwa na mdau wa michezo wilayani Rorya, Peter Owino, bingwa atazawadiwa kombe pamoja na Sh. 500,000, wa pili atajinyakulia Sh. 150,000 na seti moja ya jezi, huku wa tatu akizawadiwa seti moja ya jezi na Sh. 50,000 na mshindi wa nne akibeba mpira na Sh. 30,000.

Kocha bora wa mashindano, atazawadiwa 'tracksuit', huku mchezaji bora akiondoka na Sh. 20,000 sawa na mfungaji bora na kipa bora ambaye mbali na kiasi hicho cha fedha atapewa pia zawadi ya 'gloves', wakati mchezaji chipukizi akiondoka na kiatu. Timu yenye nidhamu itazawadiwa 'jozi 15 za 'stocking' (soksi za kuchezea mpira).

## Malindi yaachana na kocha wake

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WEKUNDU wa Mji Mkongwe, Malindi SC imetangaza kuachana na kocha wake mkuu Sheha Khamis kutokana na matokeo mabaya inayopata timu hiyo kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar.

Khamis alikuwa akiinoa timu hiyo tangu kuanza kwa msimu huu wa 2023-2024.

Akizungumza na gazeti hili jana, ofisa habari wa timu hiyo, Nassir Seif Khamis alisema kutopata matokeo mazuri hadi timu kuwepo katika mstari mwekundu wa kushuka daraja katika mzunguko wa kwanza ni miongoni mwa sababu zilizopelekea uongozi wa klabu hiyo kumpa mkono wa kwaheri kocha huyo.

Alisema katika michezo 15 waliyocheza ya mzunguko wa kwanza Malindi SC imeshinda michezo minne tu, hivyo matokeo hayo hayaridhishi kulingana na ukubwa wa timu hiyo katika Soka la Zanzibar.

Alisema baada ya kuachana na kocha huyo nafasi yake itachukuliwa na kocha msaidizi Abdulhoney Himidi Msoma ambaye alikuwamo katika benchi la ufundi la timu hiyo chini ya Khamis.

Aidha, alisema wamemwongeza kwenye benchi la ufundi Kocha Msaidizi Mohmed Suleiman "Mo" ambaye alikuwa Kocha wa Timu ya Ngome FC inayocheza Ligi Kuu ya Zanzibar.

"Uongozi wa Malindi SC katika kuongeza nguvu benchi la ufundi limemchukua kocha msaidizi Mo hivyo Msoma atasaidiwa na kocha huyo ili kuhakikisha mzunguko wa lala salama utakapoanza tunafanya vizuri na kuondoka katika mstari wa hatari," alisema Nassir.

Aidha, timu hiyo mbali na kuachana na kocha wake lakini imewapa mkono wa kwaheri wachezaji tisa wa kikosi hicho akiwemo mchezaji wa Nigeria Patrick Unjugu ambaye alidumu katika kikosi hicho msimu mmoja na nusu.

Alisema wachezaji hao waliochwa hawakuonesha viwango vizuri katika mzunguko wa kwanza hali iliyopelekea timu kuyumba na kuambulia matokeo mabaya mara nyingi kwenye michezo yao.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunaiboresha timu yetu ili mzunguko wa pili ambao ni wa walala salama tunarudi tukiwa imara," alisema Nassir.

Malindi SC ipo nafasi ya 14 katika msimamo wa ligi ikiwa na alama 15 ikishinda na michezo minne, sare tatu na imefungwa michezo nane.

## Simba Queens, Baobab hapatoshi leo Chamazi

**Na Saada Akida**

NI kivumbi leo katika mchezo wao Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara wakati Simba Queens itakapomenyana na Baobab Queens kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Katika mchezo huo, Simba Queens watakuwa wenyeji wa Baobab Queens ambao wako chini ya udhamini wa Azam.

Simba Queens wanashuka dimbani kusaka alama tatu ili kuendeleza ushindi katika michezo yao ya ligi na kuendelea kuweka hai mipango yao ya kutwaa ubingwa msimu huu.

Baobab Queens wanaenda kufuta uteja wao kutokana na misimu mitatu hawajafanikiwa kuvuna alama yoyote mbele ya Simba Queens kwenye mechi zote za nyumbani na ugenini.

Mechi mbili za msimu wa 2022, mchezo wa kwanza Baobab Queens wakiwa nyumbani walikubali kichapo cha mabao 2-0 na hata katika mchezo wa marudiano Simba Queens waliibuka na ushindi mnono wa mabao 3-0.

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema maandalizi yameenda vizuri na wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya kutafuta alama tatu muhimu dhidi ya Baobab Queens.

Alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu msimu huu kila timu imejiandaa vizuri.

"Tumejiandaa vizuri, tunafahamu haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wapinzani wetu wamejipanga na hawatakuja kama ilivyo kwa misimu mingine safari hii watakuja kivingine.

Utakuwa mchezo wa kimbinu na kiufundi kwa sababu makocha wa timu zote tunafahamiana, tunacheza kwa tahadhari na kuwaheshimu Baobab Queens," alisema Mgosi.

Aidha, aliongeza kuwa msimu huu wanahitaji kurejesha heshima ya klabu hiyo kwa kutafuta pointi tatu muhimu kila mechi ili kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa baada ya msimu uliopita kushindwa kutetea taji hilo.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa Baobab Queens, Miraji Fundi, alisema amekiandaa vizuri kikosi chake tayari kwa mchezo wao dhidi ya Simba Queens.

"Msimu huu tumejipanga vizuri na wachezaji wangu wapo tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya, tunatambua ubora wa Simba Queens, tunajipanga vizuri kuzitafuta alama tatu muhimu katika mchezo wa kesho (Leo)," alisema Miraji.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SOLANKE AWANIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mshambuliaji wa Bournemouth Muingereza Dominic Solanke mwenye umri wa miaka 26, wakati wakitafuta kusajili mshambuliaji msimu wa joto. (***Sun***)

**PHILLIPS KUTUA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United na Juventus wanaongoza kwa sasa katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Uingereza Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28 kutoka Manchester City mwezi ujao. (***Football Insider***)

**BUCHANAN AWINDWA**
INTER Milan wanasonga mbele katika mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Club Bruges wa Canada, Tajon Buchanan mwenye umri wa miaka 24 ambaye amezivutia Manchester City na Bournemouth. (***Fabrizio Romano***)

**MARTIAL BADO BADO**
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amekataa kuthibitisha iwapo mshambuliaji, Anthony Martial atauzwa Januari. (***Guardian***)



**WILLIAN KUTUA BARCA**
BARCELONA inaweza kukosa kumsajili Estevao Willian wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 16 huku Chelsea, Manchester City, Manchester United na Paris St-Germain zikijiandaa kumsajili mlinzi huyo wa Brazil. (***Mundo Deportivo***)

**WARD KUTUA MAN UNITED**
ALIYEKUWA mkurugenzi wa michezo wa Liverpool, Julian Ward ameibuka kuwa mgombea wa nafasi kama hiyo katika klabu ya Manchester United. (***Telegraph***)

**MAIA AWANIWA**
ARSENAL imemwongeza kiungo wa kati wa Sao Paulo, Pablo Maia mwenye umri wa miaka 21, kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuwindwa Januari. (***Football transfers***)

**DRAGUSIN AWINDWA**
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia Radu Dragusin baada ya kutuma maskauti kumtazama mlinzi huyo wa Romania mwenye umri wa miaka 21, akiichezea Genoa dhidi ya Juventus wiki iliyopita. (***Fabrizio Romano***)

**ILING JUNIOR AGOMBEWA**
KLABU ya Aston Villa imeungana na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumsajili winga wa Juventus, Samuel Iling-Junior mwenye umri wa miaka 20 kwa dau la takribani pauni milioni 17 huenda likatosha kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (***Football Insider***)

**FELIX KUBAKISHWA**
KLABU ya Barcelona ina nia ya kumbakisha mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24. (***Goal***)

**TAH AWANIWA WEST HAM**
KLABU ya West Ham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 27, ambaye anapendelea kuhamia Ligi Kuu ya England kuliko Bayern Munich. (***Bild***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RATCLIFFE ATAKA MASHABIKI MAN UNITED KUWA NA SUBIRA

### ●●● Awaandikia barua ya wazi kuelezea mipango ya...

**MANCHESTER,** England

SIR Jim Ratcliffe amewaandikia mashabiki wa Manchester United kuomba "wakati na subira" baada ya kuingia kwenye umiliki wa klabu hiyo.

Ratcliffe, mwenyekiti wa kampuni ya kemikali ya INEOS, amenunua hisa asilimia 25 kwa karibu pauni bilioni 1.

**Kama sehemu ya mpango huo, INEOS itawajibika kwa shughuli zote za soka, lakini Ratcliffe amewataka mashabiki kuwa na subiri kuhusu mafanikio kwani hayawezi kurejea mara moja.**

"Nilitaka kuwaandikia kwa wakati huu kutokana na jukumu muhimu la mashabiki kwa mustakabali wa Manchester United kwani tunatambua wajibu wetu kama walezi wa klabu kwa niaba yenu," Ratcliffe aliandika katika barua ya wazi kwa Manchester United.

"Ninaamini tunaweza kuleta mafanikio ya kimichezo uwanjani ili kukamilisha mafanikio ya kibiashara ambayo klabu imefurahia. Itahitaji muda na uvumilivu sambamba na ukali na usimamizi wa hali ya juu."

Kuwasili kwa Ratcliffe ni mabadiliko makubwa ya kwanza ya umiliki tangu familia ya Glazer ichukue mamlaka mwaka wa 2005.

Sir Dave Brailsford na Jean-Claude Blanc wanatarajiwa kuchukua nafasi kwenye bodi ya soka ya klabu hiyo huku wawili hao wakitarajiwa kuingia pale Carrington Januari.

Uwekezaji bado uko chini ya uidhinishaji wa udhibiti, ambao unaweza kuchukua chochote hadi wiki nane.

"Una hamu kwa Manchester United na sisi pia tunatamani," aliongeza Ratcliffe katika barua yake ya wazi.

"Hakuna uhakika katika michezo na mabadiliko yanaweza kuchukua muda lakini tuko ndani yake kwa muda mrefu na kwa pamoja tunataka kusaidia kuirejesha Manchester United mahali pake ilipo klabu.

"Tafadhali kumbuka kuwa, kama ilivyo kwa mkataba wowote, inategemea utaratibu wa kawaida wa kusaini mkataba na hivyo hatutarajii kuzungumza hadharani kuhusu masuala ya klabu hadi baada ya mkataba kukamilika."

## HABARI MICHEZO

# POCHETTINO AFICHUA KUHUSU NKUNKU

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino ametangaza nia yake ya kumtumia Christopher Nkunku katika nafasi muhimu baada ya kurejea kutoka kwenye majeruhi.

Nkunku alisajiliwa na Chelsea msimu wa joto baada ya miaka minne yenye mafanikio makubwa katika klabu ya RB Leipzig ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, lakini ilimbidi kusubiri hadi mkesha wa Krismasi kuichezea timu yake mpya kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu kutokana na jeraha baya la goti.

Jinsi Nkunku atafaa katika timu hiyo ya Chelsea imekuwa mjadala tangu kuwasili kwake na Pochettino alithibitisha kumwona Mfaransa huyo akiwa na jukumu kuu katika timu yake.

"Kwa sababu anarejea kutoka kwenye jeraha nadhani ni bora akiwa namba 10 au 9, zaidi ya kutoka upande wa kushoto au wa kulia," alisema Pochettino.

"Nadhani kwa sasa kukabiliana na mahitaji ya Ligi Kuu na kile timu inahitaji, yuko bora katika nafasi za kati."

Pochettino aliongeza: "Tunahitaji kusonga mbele kutoka kufungwa na Wolves, lakini ni vizuri kwake sasa kupata dakika na kuelewa maana ya kucheza Ligi Kuu England.

"Timu zina ukali sana na mpira wa miguu ni tofauti kabisa na nchi zingine na anahitaji kubadilika kidogo kidogo."

Nkunku alianza maisha yake ya soka akicheza mechi nyingi zaidi, lakini alionekana kuwa na ufanisi zaidi kwa klabu yake ya zamani ya RB Leipzig.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alifunga mabao 73 na kutoa asisti 53 zaidi wakati akicheza kama kiungo mkabaji au mshambuliaji kule Bundesliga.

Nyota huyo wa Ufaransa huenda akawa tayari kwa mara yake ya kwanza kuichezea klabu yake hiyo mpya baadaye wiki hii wakati Chelsea itakapomenyana na Crystal Palace katika uwanja wa Stamford Bridge.



# Kimmich ageuka lulu England

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United imeungana na Manchester City na Liverpool kwenye mchakato wa kuiwania huduma ya kiungo wa Mabingwa wa Soka nchini Ujerumani FC Bayern Munich, Joshua Kimmich, kuelekea dirisha lijalo.

Kimmich mwenye umri wa miaka 28, ni mmoja kati ya wachezaji tegemeo katika kikosi cha kwanza cha Munich, anadaiwa kuwa hana mpango wa kuondoka Januari 2024, na badala yake atasubiri hadi mwisho wa msimu huu.

Timu nyingi zimevutiwa na staa huyu ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2025.

Awali, FC Barcelona na Manchester City ndio zilionekana kuwa na uhitaji zaidi wa staa huyu lakini hivi karibuni Man United inadaiwa kuanza mazungumzo na wakala wake kuangalia uwezekano wa kumsajili.

Kimmich, ambaye alijiunga na Bayern akitokea RB Leipzig mwaka 2015, kiujumla amecheza mechi 367, akifunga mabao 41 na kutoa asisti 100.

Man United inatarajiwa kuingia sokoni kusaka majembe baada ya Sir Jim Ratcliffe kukamilisha ununuzi wa asilimia 25 za hisa za klabu hiyo.



# Man City yakaribia kumsajili Echeverri



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili chipukizi Claudio Echeverri kutoka River Plate ya Argentina, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 amevutia baadhi ya klabu kubwa Ulaya tangu alipoingia katika kikosi cha kwanza cha River Plate mwaka wa 2023, na kucheza mara sita katika mashindano yote huku wababe hao wa Argentina wakishinda Ligi Kuu ya Argentina.

Kiungo huyo mshambuliaji alivutia sana katika Kombe la Dunia la vijana chini ya umri wa miaka 17, akifunga hat-trick maarufu katika ushindi wa robo-fainali dhidi ya wapinzani wao wakuu Brazil.

90min iliripotiwa mwanzoni mwa Desemba kwamba Man City na Chelsea zimeonesha nia ya kutaka kumsajili Echeverri, na mchezaji huyo wa zamani sasa anakaribia kukamilisha dili baada ya kuendelea na mazungumzo wiki za hivi karibuni.

Makubaliano hayo yanatarajiwa kumfanya kijana huyo abaki River hadi angalau msimu wa joto, lakini anaweza kusalia hadi mwisho wa 2024 ili kupata dakika muhimu za kikosi cha kwanza.

Vyanzo vya habari vimethibitisha kwamba Man City wamesonga mbele na mazungumzo, huku pia Chelsea na Barcelona zikimwania.

Pamoja na Echeverri, 90min inaelewa kwamba Man City pia wanavutiwa na vijana wa River Plate Agustin Ruberto na Ian Subiabre pia.

Ruberto na Subiabre wote pia walivutia kwenye Kombe la Dunia la U-17 wakiwa na Argentina, huku Ruberto akitwaa tuzo ya kiatu cha dhahabu kutokana na mabao yake manane mazuri wakati wa mashindano nchini Indonesia.

Wawili hao, kama Echeverri, pia wamevutiwa na sehemu nyingine pia, huku Brighton and Hove Albion, Tottenham Hotspur, Real Madrid na Barcelona zikiwa kwenye mazungumzo.

HABARI MICHEZO

# KICHUYA KUTIMKIA JKT TANZANIA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumpoteza mshambuliaji wake tegemeo, Reliants Lusajo anayedaiwa kuwaniwa na klabu za Azam FC au Singida Fountain Gate, klabu ya Namungo huenda ikampoteza winga wake, Shiza Kichuya ambaye yuko kwenye mazungumzo na klabu ya JKT Tanzania ambayo inataka kuboresha kikosi chake kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo ya maafande wa Jeshi la Kujenga Taifa, zinasema kuwa wako kwenye mzungumzo na mchezaji huyo ili kukiongezea nguvu kikosi chao na kutekeleza maagizo ya Kocha Mkuu, Malale Hamsini, ambaye alitaka kufanyika usajili wa maana.

"Kila kitu kinakwenda sawa, muda wowote anaweza kusaini, kuna mambo ya kisheria na kimaslahi yanamaliziwa," kilisema chanzo ndani ya klabu hiyo bila kuweka wazi kama wanamsajili baada ya kumaliza mkataba wake, au watauvunja uliobaki.

Baada ya kuchapwa mabao 1-0 dhidi ya Coastal Union, Desemba 20 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, kocha Malale, pamoja kulalamika upande wa magolikipa kuwa ni dhaifu, lakini alisema atalazimika kuingia sokoni kusajili baadhi ya maeneo ambayo anaona yana upungufu.

"Tumefungwa goli jepesi, langoni kipa wetu anashindwa kuisaidia timu, kazi kubwa ya mwalimu ni kuwaelekeza wachezaji jinsi ya kutengeneza nafasi, lakini kuingiza mpira ndani ya wavu ni kazi ya mchezaji mwenyewe, utaona tumetengeneza nafasi nyingi, lakini mtu yeye na kipa au na goli anashindwa kufunga, halafu sisi tunafungwa bao rahisi vile, lakini dirisha dogo limeshafika, tunafanya usajili kuongeza wachezaji kwenye maeneo ambayo tuna upungufu," alisema kocha huyo.

Iwapo atajiunga na timu hiyo, ataungana tena na mchezaji aliyekipiga naye akiwa Simba, Said Ndemla.

Kichuya alijiunga Namungo 2020, akitokea Simba, timu ambayo aliichezea mara mbili, 2016 baadaye akauzwa Ennpi ya Misri kabla ya kurejea tena kwenye timu hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario, akipokea cheti kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, wakati wa mbio za Rombo Marathon mwishoni mwa wiki Tarakea, ikiwa na lengo la kuhamasisha utunzaji wa mazingira. Kushoto ni Mwanzilishi wa mbio hizo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Coastal Union kuwabeba wawili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Coastal Union upo kwenye mazungumzo ya kuwasajili nyota wawili, Fiston Abdulrazak na Salim Aiyee ili kukiboresha kikosi cha timu hiyo.

Fiston Abdulrazak, mshambuliaji kutoka Burundi aliyewahi kucheza Yanga anatarajia kutua nchini kwa mara nyingine kuja kuongeza nguvu ndani ya kikosi cha Wagosi wa Kaya hao.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El-Sabry, alisema wanaendelea kulitumia dirisha dogo la usajili kuimarisha kikosi chao kwa kufuata ripoti waliyokabidhiwa na Kocha Mkuu, David Ouma.

Alisema wameanza kufanyia kazi haraka ripoti hiyo kwa kuboresha kikosi chao kwa kusajili wachezaji watakaokuwa na mchango mkubwa kwenye timu hiyo.

"Tayari tuko kwenye mazungumzo baadhi ya wachezaji akiwamo Fiston, Aiyee na wengine, tunatarajji kuwasajili na wapo katika hatua nzuri za kukamilisha usajili wao," alisema msemaji huo.

Aliongeza kuwa kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi wameanza mchakato wa kufanya skauti ikiwamo kwenda visiwani Zanzibar, Kenya, Uganda na Burundi kuangalia wachezaji wenye uwezo wanaoweza kusajili.

Alieleza kuwa wanakuwa makini katika kuziba nafasi za wachezaji waliondoka na kusajili kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha duru la pili wanakuwa imara zaidi kwa kuhakikisha wanafanya vizuri.

Tayari Coastal Union imetangaza kuachana na baadhi ya nyota wao akiwamo, Frank Golubic, Balama Mapinduzi, Juma Mahadhi, Daud Mbweni na Yakubu Abdullah.

## Benchikha kuijenga timu Mapinduzi

INATOKA UK 24

Malonga mwenye miaka 21 na huyo ndiyo wanayemtaka sasa.

"Kuna mchezaji anaitwa Imoro wa Al Hilal ambaye amemaliza mkataba wake kwenye klabu hiyo, kuna mawakala walipeleka jina lake ili asajiliwe, lakini uongozi wa Simba wamemkataa kwa kuwa hawataki kusajili mchezaji huru na hata Kocha Benchikha ajahafikiana na mchezaji huyo," alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo.

Kikosi cha Simba kimeanza mazoezi jana kwenye uwanja wa Mo Arena baada ya mapumziko ya Sikukuu ya Krisimasi kwa ajili ya kujiandaa na Kombe la Mapinduzi, linalotarajiwa kuanza leo mjini Zanzibar.

Simba ipo kundi B na inatarajiwa kuingia dimbani mwaka mpya, Januari Mosi kucheza dhidi ya JKU katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar kwenye michuano hiyo.



# Michezo

Alhamisi Desemba 28, 2023
Nipashe



Ratcliffe ataka mashabiki United kuwa na subira UK. 21

# Yanga yamnasa Mcameroon

## ●●● Yamsainisha mkataba wa miaka miwili, ni mapendekezo ya...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umekamilisha dili na kuinasa saini ya mshambuliaji kutoka Klabu ya Dynamo Dougla ya Cameroon, Leonel Ateba, kwa mkataba wa miaka miwili.

Yanga imemsajili mshambuliaji huyo kwa mapendekezo ya Kocha wao Miguel Gamondi aliyetaka kusajiliwa mshambuliaji mwingine mwenye uwezo wa kufunga.

**Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe, nyota huyo atakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo inayokwenda visiwani Zanzibar katika michuanoya Kombe la Mapinduzi na kuanza mechi ya kwanza dhidi ya Jamhuri, Desemba 31, mwaka huu.**

Aidha, alisema tayari mshambuliaji huyo amemalizana na Yanga na kuja kuziba nafasi ya Fiston Mayele ambayo hadi sasa walikuwa hawajapata mrithi wake na wanaamini Ateba anakuja kukata kiu yao.

"Ateba amemalizana na Yanga na muda wowote anatua nchini kuungana na kikosi kwa ajili ya kwenda visiwani Zanzibar kwenye michezo ya Kombe la Mapinduzi, atakuwa sehemu ya kikosi na amesaini mkataba wa miaka miwili," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa ujio wa mshambuliaji huyo unawafungulia mlango wa kutokea nyota wawili, Hafiz Konkoni na Gift Freddy ambao watatolewa kwa mkopo baada ya kushindwa kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza na kushindwa kumshawishi Kocha Gamondi kuwapa namba.

Alipotafutwa Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe alisema usajili umeshafanyika (hajataja jina) na wamekamilisha kila kitu na wachezaji wao wapya wanatarajia kuonekana katika Kombe la Mapinduzi. "Tumefanya usajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi, moja ya sajili zetu tutaziona katika mechi zetu za Mapinduzi tukianza dhidi ya Jamhuri," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa kikosi cha timu hiyo kinatarajia kuondoka leo kuelekea visiwani Zanzibar na huku wakitangaza hali ya hatari kwa wapinzani wao kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Yanga wanaondoka na wachezaji wote ambao hawako katika majukumu ya timu zao za Taifa pamoja na wachezaji wapya ambao wamesajiliwa kipindi cha dirisha dogo ambalo linatarajiwa kufungwa Januari 15, 2024.



Leonel Ateba

## Benchikha kuijenga timu Mapinduzi Cup

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Abdelhak Benchikha amesema mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwake ni muhimu katika kukijenga kikosi chake kabla ya kurejea kwenye michuano ya Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa.

Benchikha amesema atayatumia mashindano hayo kuwapa mbinu wachezaji wake.

"Hii ni nafasi nzuri kwetu kuiandaa timu yetu, wiki mbili za mashindano haya zitanipa nafasi kubwa ya kuandaa timu na kuiboresha zaidi," alisema Benchikha.

Aidha, kocha huyo ametaka uongozi wa klabu hiyo kufanya usajili kwa kuboresha baadhi ya maeneo huku ikielezwa kutaka kusajiliwa beki wa pembeni kwa ajili ya kumpa changamoto naodha msaidizi, Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Inaelezwa awali Simba walikuwa na nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Mamelod Sundown, Aubrey Modiba mwenye umri wa miaka 28 lakini dili hilo limekufa.

Simba kwa sasa wamemgeukia beki wa CSMD ya Congo Brazaville, Hernest Briyock Malonga ambaye wameanza mazungumzo ya kumsajili.

Habari zilizopatikana kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi vinasema Simba imepeleka ofa kwa kutaka kumnasa beki huyo wa kushoto, huku ikimpiga chini Ibrahim Imoro aliyemaliza mkataba na Al Hilal ya Sudan kwa madai kwa sasa klabu hiyo haihitaji kumsajili mchezaji huru.

"Mpango wa kumsajili Modiba haupo, kwa sababu hakuna mazungumzo baina ya Simba na Mamelodi Sundowns kuhusu usajili wa mchezaji huyo, lakini klabu imepeleka ofa kwenye klabu ya CSMD Diables Noirs kwa ajili ya kumsajili beki wao

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

INAENDELEA UK 23